

**UPANUZI NA UBANAJI WA MAANA KATIKA KANDANDA: ULINGANISHO NA  
ULINGANUZI NCHINI KENYA NA TANZANIA**

**NA**

**ANNAH NYARANGI KIBWAGE  
C50/8112/2017**

**WASIMAMIZI**


**DR. PRISCA JERONO  
PROF. JOHN HABWE**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2023**

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na kwa maoni yangu haijawahi kuwasilishwa na mtu yeote kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada chuo kikuu chochote.


Sahihi... .....

Tarehe... 23/11/2023 .....

Annah Nyarangi Kibwage


C50/8112/2017

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi... .....

Tarehe... 24/11/2023 .....

Dr. Prisca Jerono

Sahihi... .....

Tarehe... 23/11/2023.

Prof. John Habwe

**ORODHA YA MICHORO**

Mchoro 1: Ubanaji wa Maana Kileksia.....	43
Mchoro 2: Upanuzi wa Maana Kileksika.....	44

## **IKISIRI**

Utafiti huu unahu upanuzi na ubanaji wa maana katika kadanda nchini Kenya na Tanzania. Tumebainisha kwa kulinganisha na kulinganua namna lugha ya Kiswahili inavyotumika katika utangazaji wa kandanda nchini Kenya na Tanzania, upanuzi na ubanaji wa maana za maneno katika utangazaji wa kandanda katika Kiswahili na kueleza sababu zinazopelekea kuwepo kwa mabadiliko ya kisemantiki katika lugha ya kandanda. Tumeongozwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksika katika uchanganuzi wa data yetu. Tulisikiliza matangazo ya moja kwa moja kwenye mtandao wa *YouTube* na pia kuzisoma taarifa za magazeti kuhusu mchezo wa kandanda. Imetokea kuwa kuna tofauti baina ya lugha ya kandanda inayotumika nchini Kenya na Tanzania kwa misingi ya uchanganyaji ndimi, uhawilishaji wa msimbo, matamshi ya maneno na msamiati unaotumika. Hata hivyo, inapokuja katika matumizi ya mizungu ya lugha hatupati tofauti kubwa baina ya lugha ya kandanda ya Kenya na Tanzania. Pia imedhihirika kuwa upanuzi na ubanaji wa maana hujitokeza kote Kenya na Tanzania na sababu za hali hii ni za kiisimu pamoja na mikakati ambayo imeweza kujibainisha wazi kama vile upolisemia, mazingira, urahisishaji wa mazungumzo, athari za lugha ya kwanza, analogia, utohozi, utiaji wa misamiati mipyä, kufupisha maneno na kuambatanisha maneno.

## **MAELEZO YA ISTILAHII NA DHANA**

Dhana za dharura	Hii ni dhana ambayo inaundwa mara tu msikilizaji anaposikia neno fulani.
Dhana iliyosimbwa	Hii ni maana ya kileksika iliyoko kwenye neno
Dhana inayowasilishwa	Hii ni maana ambayo inakusudiwa na msemaji katika tamko.
Michakato ya Kileksika	Hii ni mikondo ambayo leksimu hupitia ili kuibua maana au dhana mpya.
Upanuzi wa Maana	Hali ambapo neno linaongezewa maana.
Ubanaji wa Maana	Hali ambapo neno linapunguziwa maana.

## YALIYOMO

<b>UNGAMO .....</b>	<b>Error! Bookmark not defined.</b>
<b>ORODHA YA MICHORO .....</b>	<b>iii</b>
<b>IKISIRI.....</b>	<b>iv</b>
<b>MAELEZO YA ISTILAHINI NA DHANA .....</b>	<b>v</b>
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
1.1 Usuli wa Mada.....	1
1.2 Tatizo la Utafiti.....	3
1.3 Malengo ya Utafiti .....	4
1.4 Sababu za kuchagua Mada.....	4
1.5 Upeo na Mipaka.....	5
1.6 Udurusu wa Yaliyoandikwa.....	6
1.6.1 Yaliyoandikwa kuhusu Mabadiliko ya Maana .....	6
1.6 .2 Yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Pragmatiki Leksika .....	7
1.6.3 Yaliyoandikwa kuhusu Sajili .....	9
1.7 Msingi wa Kinadharia.....	12
1.7.1 Semantiki Leksika.....	12
1.7.2 Dhana za Dharura .....	13
1.7.3 Michakato ya Pragmatiki leksika .....	13
1.7.3.1 Ubanaji wa Kileksika .....	14
1.7.3.2 Upanuzi wa Kileksika .....	14
1.7.3.2.1 Upanuzi wa kisitiari .....	15
1.7.3.2.2 Chuku.....	15
1.7.3.2.3 Kisio la Maana .....	15
1.7.3.2.4 Upanuzi wa Kategoria.....	16
1.7.3.2.5 Uundaji wa Msamiati Mpya.....	16
1.8 Mbinu za Utafiti.....	16
1.8.1 Uteuzi wa Sampuli.....	17
1.8.2 Uchanganuzi wa Data .....	18
<b>SURA YA PILI .....</b>	<b>19</b>
<b>KULINGANISHA NA KULINGANUA SAJILI YA KANDANDA NCHINI KENYA NA TANZANIA .....</b>	<b>19</b>

<b>2.1 Utangulizi .....</b>	<b>19</b>
2.1.1 Umri wa mtoa ujumbe na mlengwa wa Ujumbe .....	19
2.1.2 Mbinu ya mawasiliano .....	20
2.1.3 Muktadha wa Mawasiliano .....	20
2.2 Dhana ya Sajili.....	21
2.5 Sajili ya Mchezo wa Kandanda .....	23
2.3 Lugha na Utangazaji wa Mchezo wa Kandanda.....	28
<b>2.6 LUGHA YA KANDANDA KENYA NA TANZANIA .....</b>	<b>28</b>
2.6.1 Uchanganyaji Ndimi .....	28
2.6.2 Uhawilishaji wa Msimbo .....	31
2.6.3 Nafasi ya lafudhi katika Utangazaji .....	33
2.6.4 Matumizi ya Mizungu ya Lugha .....	35
2.6.4.1 Matumizi ya Methali .....	35
2.6.4.2 Takriri .....	36
2.6.4.3 Tashbih .....	37
2.6.4.4 Tashhisi.....	39
2.6.4.5 Misemo .....	40
2.6.4.6 Maswali ya Balagha .....	40
<b>2.5 HITIMISHO .....</b>	<b>42</b>
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>43</b>
<b>3.0 UPANUZI NA UBANAJI WA MAANA NCHINI KENYA NA TANZANIA .....</b>	<b>43</b>
3.1 Utangulizi .....	43
3.2 Michakato ya Upanuzi na Ubanaji wa Maana katika Kandanda .....	43
3.2.1 Ubanaji wa maana kileksika.....	43
3.2.2 Upanuzi wa Maana Kileksika .....	45
3.2.3 Upanuzi wa kisitiari .....	46
3.2.4 Chuku.....	48
3.2.5 Kisio la Maana .....	50
3.2.6 Upanuzi wa Kategoria.....	51
3.2.7 Ubunaji wa Maana Mpya na Uundaji wa Kileksimu.....	51
3.3 Hitimisho .....	52
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>53</b>

<b>SABABU NA MIKAKATI YA MABADILIKO YA KISEMANTIKI KATIKA LUGHA YA KANDANDA .....</b>	53
4.1 Utangulizi .....	53
4.1.1 Upolisemia .....	54
4.1.2 Mazingira.....	54
4.1.3 Urahisishaji wa Mazungumzo .....	55
4.1.4 Analojia. ....	55
4.1.5 Utohozi .....	55
4.1.6 Utiaji wa Misamiati Mipyा .....	56
4.1.7 Kunyambua Maneno .....	56
4.1.8 Kufupisha Maneno/Akronimu.....	56
4.1.9 Kuambatanisha Maneno.....	57
4.1.10 Urudiaji wa Maneno.....	57
4.3 Hitimisho .....	57
<b>SURA YA TANO .....</b>	58
<b>MUHTASARI WA MATOKEO, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	58
5.1. Utangulizi .....	58
5.2. Muhtasari wa Matokeo.....	60
5.3. Mapendekezo .....	62
<b>MAREJELEO .....</b>	63

## SURA YA KWANZA

### 1.1 Usuli wa Mada

Mabadiliko ya kisemantiki katika lugha yoyote ile hujitokeza kwa namna mbili kuu ambazo ni upanuzi na ubanaji wa maana za maneno yaliyoko. Upanuzi wa maana za maneno ni badiliko la maana ambalo hutokea wakati maneno katika lugha huongezewa maana na kwa hivyo kuwa na maana nyingi kuliko hapo awali. Maana hizo mpya za maneno huwa ni tofauti na maana asilia ambazo zimezoleka kwa watu katika jamii. Kwa mfano kitenzi *shambulia* chenye maana ya kutumia kitu kama vile silaha, fimbo au ngumi ili kupiga mtu kimetanuliwa maana na kumaanisha kushindana katika kitendo au shughuli fulani ili kupata mshindi.

Upanuzi wa maana za maneno husababishwa na dhana mpya ambazo zinaendelea kuzuka au kubuniwa katika jamii. Dhana hizi mpya zinakosa maneno ya kuzitajia na kwa hivyo wanajamii hulazimika kuzipatia majina ya vitu ambavyo tayari vimo katika jamii kwa sababu ya kuwa na sifa zinazofanana au zinazoelekeea kufanana. Vitu hivi viwili ambavyo vimepewa majina sawa huwa ni tofauti kabisa kwa mfano kusema sehemu ya chupa ya kutilia kinywaji kuitwa *mdomo* na vilevile sehemu ya mwili ya binadamu na wanyama ambayo inatumika kula chakula kuitwa *mdomo*. Katika hali hii *mdomo* wa binadamu na sehemu ya chupa ya kutilia kinywaji zinachukuliwa kuwa na sifa ambazo zinafanana kutokana na kazi inayofanya, yaani kutiwa vitu.

Katika badiliko la upanuzi wa maana, maneno asilia yenyе maana maalumu huongezewa maana nyingi kulingana na muktadha wa matumizi. Katika maana hizi nyingi za neno hilo moja kunakuwa na maana ya kimsingi huku maana zingine zikiwa ni za nyongeza tu (Wamitila 2008). Kwa mfano, neno fisi ambalo lina maana ya kimsingi ya mnyama wa mwituni anayependa sana kula mizoga limepanuliwa kimaana na kupewa maana za ziada za mtu mlafi na mwanamume yejote anayetamani kuwa na wanawake wengi kimapenzi.

Kwa upande mwingine ubanaji wa maana ni badiliko la maana ambalo hutokea wakati neno ambalo lina maana nyingi linatumwiwa kuonyesha maana moja tu na kufungia maana zingine nje. Katika ubanaji wa maana sharti muktadha ambamo neno fulani limetumiwa uzingatiwe ndipo maana ya neno hilo iweze kueleweka. Shaviya (2015) anasema kuwa maana finyu inayotokana na ubanaji wa maana iwe inahusiana na muktadha wa matumizi ya neno husika. Kwa mfano

katika mchezo wa kandanda dhana ya bao humaanisha goli lililofungwa lakini katika masuala ya kimapenzi bao humaanisha kudungwa mimba.

Katika mabadiliko haya ya kisemantiki maana asilia za maneno haibadiliki bali hubaki kuwa vile vile hata kama neno litapewa maana nyingi au maana ya neno itafinywa. Anusu (2017) anasema kwamba maana asilia ya maneno husalia bila matatizo yoyote ikiwa hakuna ukinzano wowote ambao unajitokeza katika maana hizo. Kwa mfano tukisema mwanamume yule ni simba kumaanisha ni mkali kama vile simba mnyama alivyo mkali. Katika mfano huu, dhana ya ukali inayokwenda na simba vilevile itakwenda na mwanamume.

Wapo watu ambao husikiliza matangazo ya mchezo wa kandanda kupitia kwa redio au televisheni na wengine husoma taarifa zinazohusu mchezo huu katika magazeti. Wapo wanahabari ambao hutangaza mechii hizo za kandanda katika vyombo mbalimbali kwenye redio au televisheni. Utangazaji huo hufanywa kwa lugha za kimataifa, kitaifa na hata za kienyeji kwa hadhira lengwa. Watangazaji hupanua na kubana maana za maneno za lugha husika ili waweze kufikia malengo ya wasikilizaji. Utafiti huu una lengo la kuweka wazi jinsi upanuzi na ubanaji unavyotokea katika lugha ya kandanda kwa kurejelea Kiswahili.

Katika kazi hii ya utafiti, tulishughulikia ubanaji na upanuzi wa maana katika sajili ya kandanda. Dhana ya sajili iliasisiwa na mwanaisimu Halliday katika miaka ya 1960 akiwa anafuutilia yale yaliyokuwa yametajwa na waliomtangulia, hasa Firth, katika miaka ya 1950. Mwangi na Mukhwana (2011) wanasema kwamba, sajili humaanisha kaida na mikondo ya kimawasiliano itumiwayo katika hali na miktadha fulani fulani kwa madhumuni fulani maalumu.

Maneno mbalimbali huweza kutuongoza kujua sajili husika kwani msamiati mahususi ni kipengele bainishi cha kimsingi katika sajili mbalimbali. Ni kutohata na ukweli huu ambapo utafiti wetu ulijikita katika sajili ya mchezo wa kandanda huku tukichunguza namna istilahi maalumu za sajili ya mchezo wa kandanda zilivyotumiwa katika ama kubana au kupanua maana za maneno kama zinavyojulikana katika kamusi ya Kiswahili sanifu. Hili lina maana kuwa utafiti wetu utachunguza maana za msamiati mbalimbali wa Kiswahili kimatumizi kama unavyotumika katika sajili ya mchezo wa kandanda. Ufafanuzi huu una maana kuwa, sajili hutumia maneno ya kawaida na kuyapatia maana maalum inayojikita katika muktadha fulani. Kwa mfano neno *piga* lina maana ya kugonga kitu. Kwa hiyo, tunaweza kusema ‘*piga mpira*’ ambapo neno *piga* litakuwa na maana ya kimatumizi tofauti na ‘*piga mtoto*’. Hii ndiyo sababu iliyopelekea utafiti

huu kuchukua msimamo wa Crystal (1997) anayesema kuwa sajili hurejelea aina ya lugha iliyoelezwa kutegemea matumizi yake katika hali za kijamii.

Kila sajili ina sifa na sura zake ambazo zinaitofautisha na sajili zingine. Sajili ya mchezo wa kandanda kama zilivyo sajili zingine ina sifa na sura zake. Lugha ya mchezo wa kandanda inaweza kuwa ile ambayo imeeandikwa au ya kusemwa. Sajili hii ina matangazo ya michezo kwenye redio kama ripoti ya michezo iliyokwisha kuchezwa, matangazo ya moja kwa moja unapochezwa na ripoti za michezo katika magazeti. Ni kutokana na sifa hizi nyngi za sajili ya mchezo wa kandanda ambapo msamiati mwingi huenda ukapewa maana tofauti kimatumizi mbali na maana yake ya kawaida inayopatikana kwenye kamusi za Kiswahili. Katika utafiti huu hivyo basi, tulilizamia suala hili ili kuweza kubainisha ubanaji na upanuzi unaoweza kujitokeza katika sajili hii huku sababu zake zikiwekwa bayana.

Kwa kuzingatia sura na sifa hizi, tutachunguza namna ambavyo lugha ya kandanda huweza kupanuliwa na kubanwa. Kwa kuufanya utafiti huu wa upanuzi na ubanaji wa maana katika lugha ya kandanda, tutaweza kuweka wazi matumizi ya Kiswahili yanayoendana na mchezo wa kandanda. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya pragmatiki Leksika ilyoasisiwa na Blutner (1990) na kuendelezwa na Wilson (2003) na Carston (2007).

## **1.2 Tatizo la Utafiti**

Katika sajili ya mchezo wa kandanda mabadiliko ya maana za maneno asilia hutokea kwa sababu utangazaji wa mechi za mchezo wa kandanda hufanywa kwa nia ya kupitisha ujumbe kwa wasikilizaji ambao ndio hadhira lengwa. Mabadiliko haya husababisha ubanaji na upanuzi wa maana za maneno ambapo maneno hayo hupata maana mpya ambazo huweza kutofautiana kwa kiasi fulani na maana zake asilia. Ili kuweka jambo hili wazi ilibidi tujibu maswali ya kimsingi kulihusu. Je, ubanaji na upanuzi wa maana katika utangazaji wa kandanda hutokea vipi katika ulimwengu wa Kiswahili? Je, katika mifanyiko hii ya kimawasiliano ni upi ulio na athari zaidi kwa utangazaji wa kandanda katika Kiswahili na kwa nini? Majibu kwa maswali haya yalisaidia kuziba pengo ambalo tunahisi kwamba linapatikana katika utangazaji wa kandanda kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Katika utafiti huu tulilinganisha na kulinganua namna lugha ya Kiswahili inavyotumika katika utangazaji wa mchezo wa kandanda nchini Kenya na Tanzania kwa sababu hizi nchi mbili za Afrika Mashariki ndizo zilizo katika mstari wa mbele katika matumizi ya Kiswahili katika utangazaji wa kandanda. Tunafahamu tosha kwamba Kiswahili cha

Kenya na Tanzania hutofautiana kileksia na kifonolojia na fonolojia huweza kuathiri maana hasa maneno yanapotamkwa visivyo kutegemea lafudhi za wahusika na ndio maana utafiti huu ulikuwa muhimu ili kuonyesha hali hizi waziwazi kwa kuzingatia suala la ubanaji na upanuzi wa maana katika mchezo wa kandanda nchini Kenya na Tanzania.

### **Maswali ya Utafiti**

Maswali yafuatayo yalituongoza katika utafiti wetu;

1. Je, kuna ufanano na utofauti upi wa matumizi ya Kiswahili katika utangazaji wa kandanda nchini Kenya na Tanzania?
2. Je, ni mabadiliko yapi ya kisemantiki yanayoyakumba maneno ya utangazaji wa mchezo wa kandanda katika Kiswahili?
3. Je, ni sababu zifi za kiisimu na mikakati inayopelekea kuwepo kwa mabadiliko ya kisemantiki katika lugha ya kandanda?

### **1.3 Malengo ya Utafiti**

Malengo yafuatayo yalituongoza katika kuyajibu maswali yetu;

1. Kulinganisha na kulinganua namna lugha ya Kiswahili inavyotumika katika utangazaji wa kandanda nchini Kenya na Tanzania.
2. Kubainisha upanuzi na ubanaji wa maana za maneno katika utangazaji wa mchezo wa kandanda katika Kiswahili.
3. Kueleza sababu za kiisimu na mikakati inayopelekea kuwepo kwa mabadiliko ya kisemantiki katika lugha ya kandanda.

### **1.4 Sababu za kuchagua Mada**

Tafiti zimefanywa kuhusu mchezo wa kandanda na vilevile mabadiliko ya maana na wasomi mbalimbali. Kwa hivyo, tulikuwa na matumaini kwamba, baada ya kufanya utafiti huu tutaweza kuongeza maarifa katika tafiti za awali ambazo zilifanywa kuhusu mchezo wa kandanda, mabadiliko ya maana na kwa lugha ya Kiswahili kwa ujumla.

Kutokana na tajriba yetu kuhusu matangazo ya kandanda, utangazaji wa mechi za mchezo wa kandanda kupitia kwa vituo vya redio, televisheni na hata katika machapisho yakiwemo majarida na magazeti huibua maana nyingi za maneno ambazo ni mpya katika jamii. Wakati wa mawasiliano, maana hizo ambazo hazijazoleka na pengine kutofahamika kabisa na watu katika

jamii zinaweza kuleta utata katika mawasiliano na watu wakatatizika kutimiza haja za kimawasiliano. Ni muhimu kufanya utafiti huu ili kuweka hizo maana mpya ambazo zimeibuliwa wazi ili ziweze kujulikana na watu katika jamii ili kusahilisha mawasiliano katika jamii ya wazungumzaji wa Kiswahili.

Ni muhimu kufanya utafiti kuhusu mchezo wa kandanda kwa sababu umekuwa njia mojawapo ya kuunganisha watu kitaifa na kimataifa bila kujali umri, jinsia, rangi, tabaka na mahusiano baina ya watu. Kitaifa, nchini Kenya, kuna timu nydingi za mchezo wa kandanda ambazo zina wachezaji kutoka kwa jamii mbalimbali. Baada ya mechii hizi, wachezaji kutoka timu hizi huja pamoja na kujumuika au hata kuchazea timu ya taifa. Aidha, timu hizi hushabikiwa na mashabiki kutoka kwa jamii mbalimbali ambao wanajumuika nyanjani na vilabuni kuwashabikia wachezaji. Vilevile, timu hizi za Kenya hukutana na timu zingine kutoka kwa mataifa mbalimbali zikiwemo timu za Afrika Mashariki ili kuweza kushindana katika mechii hizi. Mechii hizi za kimataifa hushabikiwa na mashabiki kutoka kwa mataifa mbalimbali ambao pia hujumuika nyanjani wakati zinacheza na kwa hivyo kuwaleta watu wa mataifa mbalimbali pamoja. Ufahamu mmoja wa lugha inayotumika katika utangazajji wa kandanda utaleta maafikiano ya kimawasiliano kwa watu wanaoshabikia timu zao iwe kitaifa, kieneo au kimataifa.

Wasomi wanaendelea kufanya tafiti kuhusu mchezo huu wa kandanda na vilevile kuhusu mabadiliko ya maana za maneno katika lugha mbalimbali. Tuna matumaini kwamba, matokeo na mahitimisho katika utafiti wetu yatatumika kama marejeleo katika tafiti hizo.

### **1.5 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu ulijikita katika Kiswahili kama lugha ya utangazaji wa mchezo wa kandanda nchini Kenya na Tanzania. Tulichunguza sajili ya kandanda nchini Kenya na Tanzania ili kulinganisha na kulinganua namna lugha ya Kiswahili inavyotumika katika kubana na kupanua maana za maneno katika utangazaji wa mchezo wa kandanda. Kwa kufanya hili tulichunguza namna msamati unavyotumika katika nchi hizi mbili kwa kubana na kupanua maana za maneno yaliyopo.

Katika utafiti huu tulitegemea matangazo ya mchezo wa kandanda kutokana na yale yaliyonaswa kwenye mtandao wa *YouTube* nchini Kenya na Tanzania. Nchini Tanzania tulitumia matangazo ya *YouTube* ya vituo vya *EATV* na *Star TV*. Nchini Tanzania tulishirikisha matangazo ya mechii za timu tatu ambazo ni Simba, Yanga na Azam. Nchini Kenya tulitumia matangazo ya *YouTube*

ya vituo vya televisheni KBC na *K24* ambayo yalinaswa kwenye mtandao wa *YouTube*. Baadhi ya timu tulizoshirikisha nchini Kenya katika utafiti huu ni *Tusker*, *AFC Leopards* na *Gor Mahia*. Tulitumia matangazo ya mwaka wa 2019.

Tulisoma magazeti ya Kiswahili ambayo ni *Mwanaspoti* na *Taifa Leo* ya Tanzania na Kenya mtawalia. Kwa kila gazeti tulitumia matoleo matano matano.

Mabadiliko ya kisemantiki hasa ubanaji na upanuzi wa maana za maneno katika lugha ya kandanda yalishughulikiwa kwa upana ili kubainisha usambamba na utofauti ulioko katika msamiati wa kandanda baina ya mataifa haya mawili ya Kenya na Tanzania. Ili lilisaidia kuweka wazi Kiswahili cha Kenya na Tanzania katika muktadha wa ubanaji na upanuzi wa msamiati katika utangazaji wa kandanda kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

## **1.6 Udurusu wa Yaliyoandikwa**

Udurusu wa yaliyoandikwa ulikuwa wa yaliyoandikwa kuhusu mabadiliko ya maana, yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya pragmatiki leksika na yaliyoandikwa kuhusu sajili.

### **1.6.1 Yaliyoandikwa kuhusu Mabadiliko ya Maana**

Lyons (1968) anaeleza kwamba kinachomaanishwa pamoja na utendaji wa tamko lolote katika lugha husababishwa na jinsi tamko hilo linavyotumika katika kupashana habari na wala si utafutaji wa kinachomaanishwa na tamko hilo katika lugha hiyo husika. Katika utafiti wetu tulikuwa na lengo la kuweka wazi maana mpya za maneno zilizoibuliwa tofauti na maana asilia katika mchezo wa kandanda na kwa hivyo kuziweka wazi katika lugha ya Kiswahili kwa ujumla.

Crystal na Davy (1969) wanaeleza kwamba matumizi yoyote ya lugha hutegemea muktadha husika katika jamii. Wamezieleza sifa za sajili mbalimbali ikiwemo sajili ya michezo. Utafiti huu ultunufaisha kwa kuelewa kwa upana sifa za mchezo wa kandanda kwa sababu tuliangazia sajili ya mchezo wa kandanda. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu wao wameshughulikia sajili nydingi pamoja ilhali sisi tulijikita tu katika mchezo wa kandanda.

Rajab (2017) ameshughulikia namna maneno ya lugha ya Kiswahili yanabadilika kimaana kwa kuangazia muktadha wa kisiasa. Utafiti huu ultufaidi katika kuelewa namna mabadiliko ya maana hutokeea katika misamiati ya Kiswahili. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa ye ye alijikita katika muktadha wa siasa na sisi tulijikita katika muktadha wa kandanda.

### **1.6 .2 Yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Pragmatiki Leksika**

Okuku (2010) akishughulikia matini za fasihi ya Kiswahili amechanganua data yake kwa kutumia nadharia ya pragmatiki leksika. Ametumia michakato mitatu ya nadharia ya pragmatiki leksika ambayo ni kubanika kwa maana za maneno, kupanuliwa kwa maana za maneno na kisio la maana za maneno. Kwa sababu alifaulu kukamilisha utafiti wake, hivyo basi ulikuwa bora kwetu kwa kuwa ultipatia mwelekeo wa jinsi michakato hii ya pragmatiki leksika inavyoweza kutumika kuchanganua maana mpya zilizoibuliwa katika mchezo wa kandanda. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu alitumia michakato mitatu ambayo tumeshaitaja ilhali sisi tutatumia michakato saba ambayo ni upanuzi wa maana za maneno, ubanaji wa maana za maneno, sitiari, chuku, upanuzi wa kategoria, uundaji wa misamiati mipyä na upanuzi wa kategoria. Vilevile tulijikita katika lugha ya Kiswahili hasa sajili ya mchezo wa kandanda tofauti na alivyofanya Okuku.

Warambo (2011) ameshughulikia lugha ya Sheng huku akichunguza maendeleo ya kisemantiki katika lugha hiyo. Ameichanganua data yake kwa kutumia nadharia ya pragmatiki leksika. Katika uchanganuzi wake, aligundua kuwa maana inayowasilishwa na lugha yoyote hutokana na maneno ambayo hubeba maana hiyo na kwa hivyo ameelleza mbinu za kuunda maneno katika lugha kama vile ukopaji wa maneno kutoka lugha moja hadi nyingine, utohozi na nyinginezo. Anaendelea kusema katika uchanganuzi wake kuwa baada ya neno lolote jipya kuundwa katika lugha kutokana na mbinu ambazo amezieleza za kuunda maneno kunatokea maendeleo ya kisemantiki. Utafiti huu ni sawa na wetu ulioangazia namna maneno yanapata maana mpyä katika sajili ya kandanda na kwa hivyo kuwa ni njia moja ya maendeleo ya semantiki. Utafiti wake hata hivyo ni tofauti kwa kuwa yeye alijikita katika lugha ya Sheng ilhali utafiti wetu ulijikita katika lugha ya Kiswahili sanifu. Warambo alitumia mihimili ya pragmatiki leksika ambayo sisi pia tunatumia. Hata hivyo, Warambo alizungumzia lugha ya sheng iliyo na mizizi yake nchini Kenya kinyume nasi ambao tulilinganisha na kulinganua upanuzi na ubanaji wa maana za maneno katika mchezo wa kandanda nchini Kenya na Tanzania.

Oiro (2014) alifanikiwa kuchunguza chuku na sitiari zinazotumiwa na mwandishi katika kazi ya fasihi ili kufikisha ujumbe kwa wasomaji. Kazi yake ilitufaa katika kuielewa nadharia ya pragmatiki leksika kwa kina pamoja na michakato yake ikiwemo chuku na sitiari. Tofauti iliyoko katika utafiti wake na wetu ni kuwa, yeye alijikita katika sitiari na chuku zinazotumiwa na

mwandishi ili kuwasilisha ujumbe kwa wasomaji ambao ndio hadhira lengwa huku nasi tukiaangazia upanuzi na ubanaji wa maana za maneno katika utangazaji wa kandanda ili kubana na kupanua maana za maneno na kufanikisha mawasiliano baina ya mtangazaji na msikilizaji wa kandanda. Kwa hali hii basi, uchunguzi huu wa awali ulitumulikia namna ambavyo chuku na sitiari hujitokeza katika matangazo ya mchezo wa kandanda yaliyo ya kimazungumzo. Kwa misingi hii, tuliweza kuongezea mkabala kwa yale aliyoyasema Oiro huku akizungumzia chuku na sitiari katika kazi ya fasihi.

Simiyu (2016) amechunguza jinsi matumizi ya maneno mbalimbali yanavyoibua maana tofauti kwa hadhira lengwa na alifanikiwa kukamilisha utafiti wake kwa kutumia michakato ya nadharia ya pragmatiki leksika. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa kuwa ilituwezesha kupata ufahamu wa jinsi nadharia ya pragmatiki leksika inavyotumiwa kuchanganua maana mpya za maneno zinazoibuliwa katika lugha ya Kiswahili kwa kurejelea lugha ya mchezo wa kandanda. Mihimili ya nadharia ya pragmatiki leksika aliyoitumia Simiyu ni sawa na yetu na kwa hiyo kazi hii ilitufaa sana. Hata hivyo nyanja za utafiti zinatofautiana na kwa hiyo ufaafu wa mihimili hii iliweza kutathiminiwa kwa misingi hii.

Marisya (2017) alichanganua data yake kwa kutumia michakato ya nadharia ya pragmatiki leksika kama vile kupanuka kwa neno, kubanika kwa neno na kukisia kwa maana. Kwa kuwa mtafiti huyu ameonyesha kufaulu kwa kutumia mihimili ya nadharia hii, utafiti huu ulitufaa katika kufahamu kwa upana michakato ya pragmatiki leksika na jinsi inavyotumiwa katika kuchunguza maana za maneno kimkutadha. Utafiti wake na wetu ni tofauti kwa kuwa ye ye aliangazia sajili ya dini ilhali sisi tuliangazia sajili ya mchezo wa kandanda.

Anusu (2017) alishughulikia sababu za usawazishaji wa leksemu katika Kiswahili kwa kutumia nadharia ya pragmatiki leksika. Alibainisha namna mabadiliko ya maana za maneno yanatokea katika miktadha ya matumizi. Utafiti huu ulitufaa kwa kuelewa namna usawazishaji wa leksimu hufanyika katika lugha ya Kiswahili na mengi kuhusu nadharia ya pragmatiki leksika katika muktadha wa utangazaji wa kandanda nchini Kenya na Tanzania. Utafiti huu ni tofauti na wa sasa kwa sababu katika utafiti wetu tulieleza jinsi ubanaji na upanuzi wa maana unavyotokea katika sajili ya mchezo wa kandanda.

Okoth (2018) katika nadharia hii ya pragmatiki leksika alitumia michakato ya ubanaji wa maana, upanuzi wa maana, upanuzi wa kisitiari, chuku, kisio la maana, upanuzi wa kategoria na ubunaji wa maana mpya na uundaji wa leksimu. Kwa kuwa alifanikiwa kutamatisha utafiti wake kwa kutumia nadharia ya pragmatiki leksika katika muktadha wa magereza, utafiti wake ulitupatia mwelekeo wa jinsi ya kutumia nadharia ya pragmatiki leksika kuchanganua data katika muktadha wa kandanda pamoja na uelewa mpana wa michakato ya pragmatiki leksika kwa kuwa ndiyo tuliyoitumia katika kuchanganua data yetu. Hata hivyo, tofauti na utafiti wetu ambao unalinganisha na kulinganua matumizi ya lugha katika upana wake kwenye sajili ya kandanda nchini Kenya na Tanzania, ye ye amejikita katika matumizi ya lugha katika muktadha wa wafungwa katika jela.

Njim (2015) alichunguza namna waandishi wa habari za michezo wanavyopanua maana katika uandishi wa habari mbalimbali za michezo akiwa na lengo la kuweka wazi jukumu la muktadha katika uelewa wa dhana katika sajili ya michezo. Alichanganua data yake kwa kutumia nadharia ya pragmatiki leksika. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha kuwa kila mchezo una sajili yake na hivyo basi sifa zake mahususi za kuibainisha huku sifa mojawapo ikiwa ni upanuzi wa maana. Utafiti wake unafanana na utafiti wetu kwa sababu upanuzi wa maana ni jambo mojawapo ambalo utafiti wetu unashughulikia. Isitoshe, alitumia nadharia ya pragmatiki leksika ambayo tunatumia katika utafiti wetu kuchanganua data. Utafiti wake kwa hivyo ulitufaa kwa kuelewa zaidi kuhusu namna upanuzi wa maana unavyotokea na mengi kuhusu nadharia ya pragmatiki leksika. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na utafiti wetu kwa sababu alishughulikia upanuzi wa maana za maneno katika habari za michezo kwa ujumla katika magazeti yapatikanayo nchini Kenya.

### **1.6.3 Yaliyoandikwa kuhusu Sajili**

King'ei (2001) amechunguza sajili ya dini huku akiangazia sifa bainifu za lugha ya mahubiri kama zinavyoitokeza katika lugha ya dini katika lugha ya Kiswahili. Katika utafiti wake, aliweza kutekeleza malengo mawili ambayo ni utambuzi wa sifa bainifu za lugha ya mahubiri na utambuzi wa aina za mshikamano na jinsi zinavyounganisha mahubiri. Utafiti huu ulituwezesha kuelewa kwa upana maana ya sajili na kwa hivyo kutofautisha sajili moja na nyingine. Hata hivyo, utafiti wetu ni tofauti na wake kwa kuwa ye ye alichunguza sajili ya dini ilhali sisi tulichunguza sajili ya kandanda.

Muchura (2004) ameshughulikia namna mawasiliano yanafanikishwa baina ya mnenaji na mpokezi wa habari na jinsi mpokezi wa habari anavyoipokea na kuifasiri habari hiyo. Utafiti huu ni wa manufaa kwetu kwa sababu ulituwezesha kujua namna wasikilizaji wa mchezo wa kandanda wanavyozifasiri maana za maneno wanapokuwa wanasikiliza na kusoma matangazo ya mchezo wa kandanda. Utafiti wake hata hivyo ni tofauti na wetu kwa kuwa yeye alijikita katika sajili ya matangazo ya biashara na sisi tulijikita katika sajili ya mchezo wa kandanda.

Nandama (2004) ameangazia ubadilishaji msimbo kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kiingereza. Vile vile ameangazia sababu zinazowafanya wabunge kubadilisha msimbo na aina ya msimbo ambayo hujitokeza wabunge wanapobadilisha msimbo na ni kwa kiwango kipi ambacho wao hubadilisha msimbo. Utafiti wake ulikuwa wa manufaa kwetu kwa kuwa ameeleza maana ya sajili kulingana na wasomi mbalimbali na kwa hivyo kutuwezesha kuelewa maana ya sajili kwa upana wake. Tofauti katika utafiti wake na wetu ni kuwa yeye alitafiti sajili ya bunge na sisi tulitafiti sajili ya kandanda.

Simiyu (2010) ameshughukia ubainishaji wa nafasi ya ulinganifu wa kipragmatiki katika tafsiri ya makala ya mchezo wa kandanda magazetini katika lugha ya Kiingereza. Katika utafiti wake, amechunguza vipengee vya kiisimu na visivyo vya kiisimu vinavyoleta ulinganifu wa kipragmatiki katika mchezo wa kandanda. Ameafanua kuwa ili kubainisha ulinganifu wa kimaana uliopo baina ya matini chanzi na matini lengwa, ni sharti mchunguzi kutathmini vipengee vya kipragmatiki. Anaeleza kuwa ujenzi wa maana katika makala ya michezo unategemea zaidi vipengee ambavyo si vya kiisimu huku vipengee vya kiisimu kama vile mofolojia, sintaksia na semantiki zikiwa ni hatua tu za kufikia maana. Utafiti huu ultufaa kwa kuelewa sajili ya kandanda kwa kina kwa kuwa tulishughulikia upanuzi na ubanaji katika sajili ya kandanda. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na wetu kwa kuwa yeye ameshughulikia vipengee vya umaanisho katika lugha inayotumika katika magazeti kuripoti habari kuhusu mchezo wa kandanda nasi tulishughulika upanuzi na ubanaji wa maana katika mchezo wa kandanda na hivyo kueleza sababu zinazosababisha mabadiliko ya kisemantiki husika na athari zake kwa maana inayomfikia msikilizaji. Utafiti huu unafanana na utafiti wetu kwa sababu tulichunguza sajili ya mchezo wa kandanda sawa na alivyofanya Simiyu.

Binyanya (2014) amechunguza matumizi ya lugha ya maafisa wa polisi wanapokuwa katika eneo lao la kazi na nje ya eneo lao la kazi. Ameeleza katika utafiti wake kuwa, lugha inayotumiwa na maafisa wa polisi wanapokuwa kazini hutofautiana na ile lugha wanayoitumia wakiwa nje la eneo lao la kazi wanapowasiliana na wananchi. Kwa kusoma utafiti huu, tuliweza kuelewa kwa upana jinsi lugha inavyotofautiana kutoka eneo moja hadi lingine. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwa sababu yeye aliangazia sajili ya maafisa wa polisi na sisi tuliangazia sajili ya mchezo wa kandanda.

Humpolik (2014) ameichunguza lugha ya kandanda kwa kujikita katika watangazaji wa mpira wa kandanda wa Uingereza. Lengo la utafiti wake lilikuwa kuwasilisha matangazo ya mpira wa kandanda kama sajili inayojitegemea na iliyokamili, kuichanganua na kubainisha sifa zake. Matokeo yake ya utafiti yalionyesha kuwa muundo wa ndani wa sajili ya matangazo ya mchezo wa kandanda unatofautiana kutegemea watangazaji, shinikizo na muda walio nao. Mawazo haya yatakuwa muhimu kwa kasi yetu ya utafiti ambayo inachunguza upanuzi na ubanaji wa maana katika mchezo wa kandanda lakini kwa kurejelea lugha ya Kiswahili.

Budejovice (2015) alikuwa na lengo la kubainisha matumizi ya upolisemia na homonimia katika matangazo ya mchezo wa kandanda. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa lugha ya mchezo wa kandanda inapitia mabadiliko ya kisemantiki huku vipengele vya upolisemia na homonimia vikijitokeza kwa wingi kama sifa bainifu. Mwandishi huyu alijikita katika lugha ya Kiingereza na hii ndiyo tofauti ya kimsingi baina ya kazi yake na yetu. Isitoshe, upeo wetu ni mpana kwa kuwa tunachunguza utangazaji wa kandanda katika nchi mbili tofauti na ambazo ni Kenya na Tanzania. Mfanano uliopo baina ya kazi hii na yetu ni kwamba, zote zinachunguza mabadiliko ya kisemantiki katika mchezo wa kandanda.

Otieno (2015) amechunguza matumizi ya lugha katika anwani zinazoripoti kuhusu michezo nchini Kenya. Alilenga kuchunguza lugha inayotumiwa katika mchezo wa kandanda wakati wa kusimulia matukio ya kandanda katika utafiti wake. Alijikita katika kubainisha lugha ya vita inavyotumiwa katika kueleza matukio ya mchezo wa kandanda katika magazeti yapatikanayo nchini Kenya. Matakeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa lugha inayotumiwa katika magazeti kueleza mpira ni lugha inayodhihirisha miktadha ya vita na mapambano. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu upeo wake ni finyu ukilinganishwa na wetu. Mfanano uliopo ni kwamba

ameangazia magazeti ya nchini Kenya na ambacho ni kipengele mojawapo kinachochunguzwa na kazi hii ya sasa.

### **1.7 Msingi wa Kinadharia**

Katika utafiti huu nadharia ya Pragmatiki Leksika ilituongoza kwa sababu ni faafu kwa kuwa inachanganua maana za maneno kwa kutegemea muktadha wa matumizi wa maneno hayo. Nadharia hii iliasisiwa na Blutner (1990). Nadharia hii iliweza kuelezwa zaidi na Wilson (2003) na Wilson & Carston (2007). Mihimili ya nadharia hii ni mingi lakini tulitumia ile ambayo ilitufaa katika kuchanganua data katika utafiti huu.

Nadharia ya pragmatiki leksika inachunguza jinsi maana ya neno hufasiriwa kulingana na muktadha wa matumizi ya neno hilo na kwa hiyo ni nadharia inayofaa katika uundaji wa dhana za dharura ili kuelewa maana inayokusudiwa. Hii ni kwa sababu matumizi ya maneno katika lugha yoyote ile huwa tofauti tofauti kulingana na muktadha husika.

Maelezo haya ya nadharia ya pragmatiki leksika yalikuwa muongozo muhimu katika utafiti wa sasa ulioleza msamiati uliotumiwa katika lugha ya Kiswahili kutangaza mchezo wa kandanda. Msamiati huo ulichunguzwa kwa maana yake ya kamusi na uliyozoleka kisha kutathminiwa kwa maana yake kimuktadha na hivyo kubainisha upanuzi au ubanaji wa maana ya neno husika. Muktadha ulikuwa kipengee muhimu katika kupata maana za maneno mbalimbali yaliyopatikana katika data ya utafiti huu. Ifuatayo ni mihimili ya nadharia ya pragmatiki leksika na ambayo ilikuwa na umuhimu mkubwa katika uchanganuzi wa data ya utafiti huu.

#### **1.7.1 Semantiki Leksika**

Semantiki leksika ni mhimili wa nadharia ya pragmatiki leksika ambao hujishughulisha na maana ya neno. Kulingana na mhimili huu, maana yoyote ya neno hutokana na vile neno hilo limetumika katika muktadha husika ili kufanikisha mawasiliano Mhimili huu ulimnufaisha mtarufi kwa sababu alipata maneno mbalimbali na kuyaweka katika vikoa maana tofauti tofauti.

Maneno ambayo yaliwekwa katika kikoa maana kimoja yalichukuliwa kuwa yanahusiana kimaana. Mtarufi aliyatambua maneno ambayo yamepata maana mpya kupitia kwa vikoa maana. Vikoa hivi vilimsaidia mtarufi kuweza kubainisha maneno mbalimbali yaliyotumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda ambayo maana zao zilipanuliwa au zilibanwa.

### **1.7.2 Dhana za Dharura**

Dhana za dharura ni mhimili wa nadharia ya pragmatiki leksika ambao unajishughulisha na uundaji wa dhana za dharura ili kufanikisha mawasiliano baina ya mnenaji na mpokezi wa ujumbe. Wakati wa kujaribu kuelewa tamko, msikilizaji wa ujumbe hulazimika kuunda dhana za dharura ili aweze kuufasiri ule ujumbe ambao mneneji anaudhamiria. Uundaji huu wa dhana za dharura huundwa kwa kuzingatia muktadha wa mazungumzo ambao unahusika kwa kuwa tamko moja katika lugha yoyote ile husika huweza kutumika kuibua maana tofauti tofauti katika miktadha mbalimbali. Kwa mujibu wa Horn na Ward (2004) dhana ya dharura huundwa wakati wa tukio na hakuna uwezekano kuwa mtu ye yoyote alishaiunda dhana hiyo ya dharura tayari ili iweze kutumika katika mawasiliano.

Udharura husababisha hali ya kudumu kwa sababu maana zilizopanuliwa na kutumika kwa lugha ya Kiswahili husalia kuwa maana mpya ambayo baadaye huzoleka na kutumika mionganini mwa watu. Kwa mfano, hali ya kuwa mchawi ni dhana inayojitokeza katika mchezo wa kandanda kwa maana ya mtu aliye stadi au fundi kama ambavyo mtu anayetajika katika urogi ataitwa vile vile.

Mhimili huu wa dhana za dharura utakuwa muhimu katika utangazaji wa mchezo wa kandanda hasa kuto kana na matangazo ya mchezo wa kandanda yaliyonaswa na kuhifadhiwa na vyombo vya habari kwenye mtandao wa *YouTube* ambao ndio uliotumika kama njia ya kimsingi ya kutupatia data ya utafiti huu. Hii ni kwa sababu, wakati msikilizaji anasikiliza matangazo hayo huwa na lengo la kupata ujumbe ambao unadhamiriwa na mtangazaji. Kwa kuwa mchezo huu mara nyingi, huwa wa kasi hali hii hulazimisha msikilizaji kuunda dhana za dharura ili aweze kuufasiri ujumbe wa mtangazaji kwa haraka ili aendane sambamba na mchezo huo.

Mbali na mihimili hii miwili kutumika katika uchanganuzi wetu wa data, tumetumia pia michakato mbalimbali inayotumika katika kufanikisha matumizi ya nadharia ya pragmatiki leksika.

### **1.7.3 Michakato ya Pragmatiki leksika**

Ili kuweza kufanikisha matumizi ya nadharia ya pragmatiki leksika katika uchanganuzi wa data yetu mifanyiko na michakato fulani fulani huweza kufuatwa. Michakato hii imeelezwa hapa chini.

### **1.7.3.1 Ubanaji wa Kileksika**

Kulingana na Wilson (2003) ubanaji wa maana za maneno ni badiliko ambalo linahusisha matumizi ya tamko ili kuwasilisha maana maalumu ya tamko ikilinganishwa na ile ambayo imesimbwa kisemantiki na neno hilo na hali hii hufanya maana thabiti ya neno hilo kiisimu kubanwa. Mtafiti anaongezea kuwa katika mchakato wa ubanaji maana nyingi ya neno huachwa nje na maana moja hutawala katika muktadha wa matumizi. Badiliko hili linapotokea katika mawasiliano yoyote yale katika jamii, maana finyu ya neno huwasilishwa kuliko ile ambayo neno hilo limesimba kisemantiki katika lugha husika. Kwa mfano, neno *mchawi* lina maana ya mtu anayeaminika kuwa hodari kwa kutumia ushirikina na kusababisha maafa. Katika muktadha wa kandanda, tukisema Arocho ni *mchawi* tuna maana ya kuwa Arocho ni hodari kwa kuchenza kandanda na kwa hivyo maana ya kutumia ushirikina na kusababisha maafa yanafungiwa nje katika muktadha huu.

Hili ndilo tulitolifanya katika utafiti wetu kwa kuyachunguza maneno yaliyobanwa ili kuonyesha umahususi wa matumizi ya maneno hayo kuliko yaliyosimbwa kisemantiki katika utangazaji wa mchezo wa kandanda na kuyaweka wazi katika Kiswahili.

### **1.7.3.2 Upanuzi wa Kileksika**

Upanuzi wa kileksika ni hali ambapo neno linatanuliwa kimaana na kuwa na maana nyingi ikilinganishwa ilivyokuwa hapo awali. Maana ya awali ya neno hilo ambalo limetanuliwa inakuwa ndiyo maana ya kimsingi na maana nyingine ambayo imeongezwa katika neno hilo zikiwa ni za nyongeza tu. Kwa mfano; Timu ya AFC Leopards *ilicharaza* timu ya Wazito FC mabao 5-2. Neno *charaza* lenye maana yake asilia kulingana na kamusi ya lugha ya Kiswahili ya kupiga kwa mfululizo ngoma, kinanda au fimbo maana yake imetanuliwa katika utangazaji wa kandanda na kumaanaisha kitendo cha timu moja kufunga timu nyingine mabao mengi na kwa hivyo kuibuka washindi.

Katika mchakato huu wa upanuzi wa kileksika neno moja linaweza kutumika katika miktadha mbalimbali na kuibua maana tofautitofauti. Katika utafiti huu tuliyachunguza maneno yaliyopewa maana za ziada ili kufanikisha mawasiliano baina ya msemaji na msikilizaji na hivyo maana zao kupanuka kimatumizi kwa kurejelea muktadha wa mchezo wa kandanda.

#### **1.7.3.2.1 Upanuzi wa kisitiari**

Kuhusu kipengele hiki cha upanuzi wa maana za maneno, Anusu (2017) anasema kwamba badiliko hili hutokea wakati ambapo tamko ambalo linatumika kuonyesha fikra fulani kwa njia iliyo wazi linatumika pia kuonyesha fikira ambayo inafanana kwalo. Tunakubaliana na maelezo haya na kuongezea kuwa, katika mchakato huu, maana ya tamko katika eneo la mazungumzo linalohusika hutofautiana kwa kiwango kikubwa na maana inayojulikana ya tamko hilo kwa kuwa maana inayohusishwa inahamishwa kutoka kwa kitu kimoja hadi kwa kitu kinginecho.

Katika mchakato huu msemaji anaweza kufananisha mtu na mnyama. Hadhira lengwa nayo inalazimika kukisia maana iliyosimbwa na kukisia huko kunaweza kuwa ukweli kwa kile msemaji alikuwa anamaanisha au si ukweli. Kwa mfano, mtangazaji wa mchezo wa kandanda kusema *Messi ni simba*. Simba ni mnyama anayejulikana kuwa mkali kuliko wanyama wote porini. Neno hili linapotumika katika muktadha wa mchezo wa kandanda msikilizaji alazimika kukisia maana na kusema Messi ndiye mchezaji bora kuliko wote katika mechii hiyo. Hivi ndivyo tulivyotumikiza dhana ya upanuzi wa kisitiari kwa kurejelea matangazo ya mchezo wa kandanda.

#### **1.7.3.2.2 Chuku**

Kuhusu kipengele hiki cha upanuzi wa maana, Wilson (2003) anasema kuwa hili ndilo badiliko la upanuzi wa maana ambapo maana za maneno zinatanuliwa kwa hali ya juu na kunatokea tofauti kubwa kati ya maana asilia na maana inayodhamiriwa wakati wa mawasiliano.

Katika aina hii ya upanuzi wa maana za maneno, maneno hutiwa chumvi na kupigwa chuku na maana zao haichukuliwi kijujuu. Kwa mfano, Juma ni mwalimu *hatari* kwa kufundisha Kiswahili. Neno *hatari* limetumika kutia chumvi ufunzaji mzuri wa mwalimu Juma.

Maelezo haya yaliufaidi utafiti huu katika kueleza namna utangazaji wa mchezo wa kandanda ulivyoweza kuongeza chumvi au kupiga chuku ulipoeleza hali ilivyo au ilivyokuwa au itakavyokuwa uwanjani kabla, wakati wa au baada ya mchuano.

#### **1.7.3.2.3 Kisio la Maana**

Katika badiliko hili la upanuzi wa maana tamko ambalo lina maana madhubuti linatanuliwa mwishoni mwake na kuweka pamoja hali mbalimbali ambazo ziko nje ya maana madhubuti ya

tamko hilo kiisimu katika lugha husika. Katika badiliko hili, kuna tofauti kubwa sana kati ya maana asilia ya tamko na ile maana ambayo inawasilishwa katika tamko, Wilson (2003).

Kwa mfano mwanafunzi aliye kosa kuhuduria somo fulani anapouliza mwenzake ni wanafunzi wangapi walihuduria somo atamjibu ni *wanafunzi wengi* hata kama darasa lao lina wanafunzi kumi. Katika hali hii mwanafunzi aliye kosa kuhuduria atakisia maana ya wengi na kusema kwamba huenda yeye pekee ndiye hakuhuduria somo. Kutokana na huu mfano, maana ambayo inawasilishwa huwa tofauti kabisa na maana iliyosimbwa kiisimu.

Hili ndilo tumelifanya katika utafiti huu kwa kuyachunguza maana za maneno zinazokisiwa na wasikilizaji wakati wa utangazaji wa mchezo wa kandanda.

#### **1.7.3.2.4 Upanuzi wa Kategoria**

Katika badiliko hili la upanuzi wa maana, nomino za kipekee na nomino za kawaida ndizo ambazo huchangia katika kupanua maana. Katika soka tunaweza kupata majina kama vile Messi wa Afrika kwa maana ya mchezaji kutoka bara la Afrika anayecheza vizuri sana kama Messi Muajentina. Hili ndilo tumelifanya kwa kuyachunguza maneno ambayo yamepanuliwa kategoria katika utafiti wetu.

#### **1.7.3.2.5 Uundaji wa Msamiati Mpya**

Uundaji wa msamiati mpya ni mfanyiko ambao unahusu kujitokeza na maneno mapya au kuongeza viambishi vya awali au tamati katika leksimu ambazo tayari zipo katika lugha fulani na kusababisha kujitokeza kwa maana mpya kwa msamiati huo husika na vilevile kupanua maana au kubana maana za maneno yaliyopo katika lugha husika. Kwa mfano kusema, Mababe wa KPLC waanza matayarisho ya FKF.

Mfanyiko huu unaohusu uundaji wa msamiati mpya katika lugha unahusu vilevile kuleta maneno mawili ambayo yana maana zao za kimsingi ambayo yapo katika lugha husika na kuyaunganisha ili kuunda neno moja ambalo lina maana tofauti. Kwa mfano *mwanakandanda* kwa maana ya yule anayeshiriki kandanda kama mchezaji. Hili ndilo tulilolifanya kwa kuangazia maneno mwambatano katika lugha ya kandanda nchini Kenya na Tanzania.

### **1.8 Mbinu za Utafiti**

Utafiti huu ni wa maktabani. Mtafiti alisikiliza matangazo ya moja kwa moja ya awali ya mchezo wa kandanda katika mtandao wa *YouTube* ndipo alindondoa data na kuzichambua.

Aidha, mtafiti alizisoma taarifa za magazeti kuhusu mchezo wa kandanda na kunakili data kisha baadaye kuichanganua.

Katika utafiti huu, dhana ya utangazaji na utangazaji ni visawe. Hata hivyo, dhana ya kimsingi ambayo ni utangazaji inahusu upashaji wa habari kutoka chanzo hadi hadhira lengwa. Kwa misingi hii basi, dhana ya utangazaji inatumika katika upana wake na wala si ufinyu unaokwenda na kutolewa kwa sauti katika vyombo vyaa habari hii ni kumaanisha kuwa, utangazaji kama dhana ilitumika katika kazi hii kurejelea upashaji wa habari kutoka kwa vyombo vyote vyaa habari.

### **1.8.1 Uteuzi wa Sampuli**

Sampuli ya kimakusudi ilitumiwa katika utafiti huu. Sampuli hii ilihuisha gazeti la Tanzania ambalo ni *MwanaSpoti*. Gazeti hili ni miuongoni mwa magazeti yanayoeleza kimaandishi mchezo wa kandanda nchini Tanzania na huweza kuuzwa katika nchi jirani kukiwemo Kenya. Vilevile gazeti hili hupatikana kwenye mtandao na kwa hiyo, liliweza kusomwa kirahisi na mtafiti. Pia, tulilisoma gazeti la Kenya ambalo ni *Taifa Leo*. Kwa kulisoma gazeti la Tanzania na Kenya, tumeweza kulinganisha na kulinganua jinsi mabadiliko ya kisemantiki katika lugha ya Kiswahili yanajitokeza kwa kuchunguza matangazo ya mchezo wa kandanda.

Magazeti ya mwezi wa Septemba na Oktoba mwaka wa 2019 yalitumika. Kwa kila gazeti, tulitumia matoleo matano na yaliyopipoti mchezo wa kandanda uliochezwa wikendi. Wikendi ni wakati muhimu kwa mtazamaji na usikilizaji wa matangazo ya mchezo wa kandanda kwa sababu ni wakati wa mapumziko usiokuwa wa kufanya kazi. Uteuzi huu ulifanywa kimakusudi ili kupata data toshelevu tuliyohitaji kwa ajili ya utafiti wetu. Magazeti haya yalikuwa yale ya upeo wa juu wa msimu wa kandanda ulimwenguni kote kwa kuwa kalenda ya kandanda ulimwenguni huthibitiwa na FIFA. Tuliamini kuwa matoleo matano ya kila moja katika magazeti haya yatatupatia data ya kutosha kwa ajili ya utafiti wetu.

Matangazo ya mechi yanayozihusu timu za mchezo wa kandanda kwenye mtandao wa *YouTube* yalisikilizwa. Matangazo ya vituo vyaa televisheni yaliyopeperushwa moja kwa moja na kunaswa kwenye mtandao wa *YouTube* ndiyo yatakayosikilizwa. Nchini Tanzania tutatumia matangazo ya *YouTube* ya vituo vyaa *EATV* na *Star TV*. Nchini Tanzania, tulishirikisha matangazo ya mechi za

timu tatu ambazo ni *Simba*, *Yanga* na *Azamu*. Tulizichagua timu hizi kwa sababu zina matokeo mazuri katika ligi kuu. Tuliyatumbia matangazo ya mwaka wa 2019.

Pia, matangazo ya mechi za timu za Kenya katika vituo vya televisiuni vya KBC na *K24* ambayo yalinaswa kwenye mtandao wa *YouTube* mwaka wa 2019 yalisikilizwa. Baadhi ya timu tulizoshirikisha nchini Kenya katika utafiti wetu ni *Tusker*, *AFC Leopards* na *Gor Mahia*. Timu hizi ziliteuliwa kimakusudi kwa sababu ni pinzani na zinajitokeza katika nafasi za mwanzo katika ligi. Hali hii imezifanya timu hizi kuwa na watu wengi wanaopenda kusikiliza matangazo ya mechi zake. Tutasikiliza michezo mitatu kwa kila timu tuliyochagua kimakusudi na tuliamini kwamba michezo hiyo mitatu itatupatia data ya kutosha ili kufanikisha utafiti wetu.

### **1.8.2 Uchanganuzi wa Data**

Data tuliyoikusanya na kuinakili kutoka kwenye mtandao wa *YouTube* na maktabani imeanishwa kwa kuzingatia vipengele mbalimbali kama vile msamiati na istilahi. Tumeipanga data hiyo tuliyoiipata na kuichanganua ili kutambua maana zilivyoimbwa na kuwasilishwa. Mihimili ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika imetuongoza katika uchanganuzi wa data ili kubainisha maana. Isitoshe, maswali na malengo ya utafiti huu kama tulivyobainisha yametumika kupata mwongozo kamili wa uchanganuzi wa data husika tuliyoikusanya. Tumetumia maelezo kuchanganua data yetu.

## **SURA YA PILI**

### **KULINGANISHA NA KULINGANUA SAJILI YA KANDANDA NCHINI KENYA NA TANZANIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Katika sura iliyotangulia hii, tumeweza kuzungumzia usuli wa mada, tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti wetu, sababu za kuchagua mada hii, yaliyoandikwa kuhusu mada hii, msingi wa kinadharia na mbinu za utafiti.

Katika sura hii tumeeleza mambo yanayofanikisha mawasiliano na dhana ya sajili. Kwa sababu utafiti wetu unahu su sajili ya mchezo wa kandanda, katika dhana ya sajili tumeeleza sifa na sura za sajili ya mchezo wa kandanda. Vilevile sura hii imeeleza mifanano na tofauti zilizopo baina ya lugha ya kandanda nchini Kenya na Tanzania kwa namna ambavyo imejidhihirisha kutokana na mbinu zetu za utafiti. Hii ni kwa sababu nchi za Kenya na Tanzania zina historia tofauti ya sera na matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Ijapokuwa tunazungumzia lugha ya kandanda ni vyema kutaja, japo kwa ufupi mambo yafanikishayo mawasiliano katika jamii. Baadhi ya mambo yametumikizwa katika lugha ya kandanda katika sura za baadaye katika tasnifu hii. Mambo haya ni kama yafuatayo:

#### **2.1.1 Umri wa mto ujumbe na mlengwa wa Ujumbe**

Umri wa mto ujumbe na mpokeaji sharti uzingatiwe katika mawasiliano yoyote katika jamii. Kwa mfano, mtu mkubwa anapowasiliana na mtoto mwenye umri mdogo lazima atumie ishara na misamiati ambayo mtoto anaolewa ili afanikishe mawasiliano. Aidha, wazee katika jamii

huzungumziwa na watu wenye umri mdogo au wa makamo kwa njia ya heshima huku miko yote inayokwenda na lugha husika ikizingatiwa Kwa mfano mtangazaji anaposema mchezaji fulani amepigwa na mpira pabaya mtoto hataelewa kama pabaya ni wapi na ndio maana suala la umri ni muhimu katika mawasiliano. Kwa kutumia lugha kama hii, mtangazaji atataka asivunje mbeko na miko inayokwenda na lugha ya Kiswahili bila kujali umri.

### **2.1.2 Mbinu ya mawasiliano**

Hii ni njia inayotumika kutuma ujumbe kutoka kwa mtu mmoja hadi mwengine. Mto ujumbe anaweza kutuma ujumbe kwa hadhira lengwa ana kwa ana, kupitia kwa vyombo vya habari kama vile redio, televisheni, magazeti, majarida, vitabu, mapango na barua au kwa kutumia ishara zilizozoleka na jamii lugha husika. Vivyo hivyo, mtangazaji wa kandanda atatumia lugha kwa njia ya mazungumzo au maandishi ili kufikia hadhira lengwa yake ikiwa wamezoea mazungumzo au maandishi. Kwa hali hii, maneno atakayotumia mtangazaji au mwandishi wa habari za mchezo yataonyesha na kudhihirisha ubanaji au upanuzi wa maana za maneno.

### **2.1.3 Muktadha wa Mawasiliano**

Muktadha ni mazingira maalumu ambayo humhitajia msemaji au mtu anayewasiliana kutumia lugha maalumu inayojitofautisha na aina nyingine yoyote ile ya lugha. Tukirejelea msamiati, tunaweza kusema kuwa muktadha ni mazingira ambamo neno fulani linatumika ili kuibua maana maalumu. Muktadha wa mawasiliano unaweza kusababisha maana ya neno moja kuwa na maana nyingi kwa mfano katika mchezo wa kandanda tunaposema Arocho ni mchawi tuna maana kuwa yeze ni hodari wa kusakata mpira.

Kuhusu suala hili la muktadha, Wavriner na Francis (1977) wanasema kuwa kuna aina mbili za muktadha ambazo ni muktadha wa hali halisi na muktadha wa kiisimu. Muktadha wa hali halisi ni mazingira fulani ambamo matumizi ya neno hutokea kwa wakati fulani. Hii ina maana kuwa, katika mkutadha wa hali halisi kama msikilizaji hajakuwa katika hayo mazingira na kushuhudia vitendo vilivyofanyika, itakuwa vigumu kuelewa kile ambacho kinazungumziwa. Msikilizaji ili aweze kuelewa tamko katika muktadha huu wa hali halisi anahitajika kuwa na uelewa wa matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali kwa kujifunza kwa sababu kujua matumizi ya neno katika muktadha mmoja kutaleta matatizo katika mawasiliano na kusababisha kutatizika kutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii kwa sababu ya kukosa kuelewa ujumbe. Hali hii

ni dhahiri katika mfano tulioutoa hapo juu ambapo mchawi kikawaida huwa ni mtu wa kuwadhuru watu kwa kutumia marogo yake.

Muktadha wa kiisimu nao ni mazingira ambamo aina za maneno kwa kawaida hutumika na yanaweza kukisiwa maana. Katika aina hii ya muktadha, si lazima mpokezi wa ujumbe ashiriki katika matendo au shughuli ambayo inahusika ndio aweze kuelewa maana. Kwa mfano, neno chai linapotumika katika kandanda humaanisha hongo hasa kwa upande wa refa au wasaidizi wake.

## **2.2 Dhana ya Sajili**

Dhana ya sajili au kwa jina jingine rejesta kama tulivyotaja hapo awali iliasisiwa na mwanaisimu Halliday katika miaka ya 1960 akiwa anafuutilia yale yaliyokuwa yametajwa na waliomtangulia hasa Firth katika miaka ya 1950. Sajili kwa mujibu wa Iribemwangi na Mukhwana (2010) humaanisha kaida na mikondo ya kimawasiliano itumiwayo katika hali na miktadha fulani fulani kwa madhumuni fulani maalumu katika taaluma ya isimujamii na mawasiliano. Wanaendelea kusema kuwa sajili hujishughulisha na jinsi lugha inavyotumika katika hali mbalimbali na kwa sababu hii sajili ni ubadilishaji wa utaratibu wa matumizi ya lugha kutegemea namna inavyotumika katika miktadha mbalimbali ya kihali.

Iribemwangi na Mukhwana (2010) huku wakizungumzia suala la sajili wanamuunga mkono mwasisi wa sajili Michael Halliday (1960) ambaye anasema kuwa suala zima la sajili huathiriwa na mambo matatu ambayo ni:

1. Eneo au uwanja unaozungumziwa. Suala hili linahusu mada inayozungumziwa na inakozungumziwa kwa kuwa kila mada huhitaji msamiati fulani maalumu na hata namna ya kuutumia.
2. Mtindo au namna. Hii ni namna ya kufanya jambo.
3. Utaratibu wa mahusiano ya maisha. Huu ni uhusiano baina ya mse maji na msikilizaji kwa mfano uhusiano baina ya mwalimu na mwanafunzi au mgonjwa na daktari.

Kulingana na Crystal (1977) sajili ni aina ya lugha kutegemea matumizi yake katika hali za kijamii kutokana na mtindo fulani wa matumizi ya lugha na muktadha wake. Watumiaji wa lugha wanahitajika kuitumia lugha katika hali na miktadha fulani na wala si kutumia lugha ile ile

kote kote. Maelezo haya yana maana kwamba lugha inayotumiwa katika mazishi ni tofauti na ile lugha ambayo inatumika kanisani au katika kutangazia mchezo wa kandanda kwa sababu miktadha hii ni tofauti na kwa hivyo lugha inayotumika haiwezi kuwa sawa. Lugha ya mazishi itakuwa ni ya kuomboleza na kuwafariji waliofiwa ilhali lugha ya kandanda itakuwa lugha ya mihemko na tahiruki pamoja na utiaji mbwembwe.

Katika jamii kuna kazi mbalimbali wazifanyazo watu kama vile kazi ya ualimu, kazi ya ukulima, uhandisi, uanasheria, polisi na kuhubiri. Watu wanapozifanya kazi hizi huwa na uelewa wa jinsi ya kutofautisha lugha wanayoizungumza wakiwa kazini na wanapokuwa hawako kazini. Tukichukulia mfano wa mwanasheria akiwa kazini na wanasheria wengine watatumia lugha yenye msamiati kama vile kesi, mashtaka, mshtakiwa na kifungo lakini watu hao wanapokuwa nje ya kazi zao wanazungumza lugha ambayo ni tofauti sawa na kwa mwalimu na mwanafunzi wakiwa shulenii na nje ya eneo la kazi hiyo. Maelezo haya yanafanana na ya Trudgil (1974) anayesema kuwa kazi mbalimbali wazifanyazo watu huwa ndio msingi wa ile lugha watakayoitumia. Crystal na Davy (1969) kwa upande mwingine wanasema kuwa matangazo ya michezo, matangazo ya biashara, mada kuu za magazeti, ibada za kanisani ndivyo vitu ambavyo vinastahili kuitwa sajili.

Kutokana na maelezo haya mbalimbali tunapata sifa za sajili. Kwanza, kila sajili inatumia msamiati wake maalumu ambao unaitofautisha na sajili nyingine. Hii ina maana kuwa neno moja au mawili yanatosha kwa mtu ye yeyote anayechunguza lugha kutambua aina ya sajili inayohusika kama ni sajili ya kandanda, bunge, shulenii, kanisani na hospitalini. Kwa mfano sajili ya hospitalini itatumia msamiati kama vile, dawa, mgonjwa, matibabu, na kwa hivyo kuwa rahisi kuitambua aina hii ya sajili.

Pili, sajili hutambulishwa na aina za sentensi ambazo zinatumika katika sajili husika na watumizi wa lugha. Kuna sajili ambazo zinatumia sentensi fupi fupi na sajili zingine zinatumia sentensi ndefu ndefu. Sajili ya mchezo wa kandanda kwa mfano hutumia sentensi ambazo ni fupi fupi kwa sababu mchezo huwa wa kasi na mtangazaji anataka kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa na kwa hivyo mtangazaji hana wakati wa kutunga sentensi ndefu ndefu. Hii ni tofauti na ilivyo katika sajili ya bunge na sheria ambapo sentensi zinazotumika ni zile ndefu ndefu ili kuwasilisha ujumbe.

Aidha, sajili yoyote ile haiwezi kutenganishwa na muktadha. Muktadha ni mazingira ambamo shughuli tofauti tofauti hutekelezwa kwa kutumia lugha. Jinsi shughuli hizo zilivyo tofauti ndivyo matumizi ya lugha yanakuwa tofauti na kwa hivyo kusababisha aina mbalimbali za sajili au rejestra.

Isitoshe, kila sajili huwa na viambata lugha ambavyo huweza kutofautiana kutoka sajili moja hadi nyingine. Hivi viambata lugha huendana na matumizi ya ishara za kimwili, nyimbo na hata rangi. Kwa mfano, lugha ya tanzia itaambatana na nyimbo za faraja pamoja na usomaji wa maandiko matakatifu.

## **2.5 Sajili ya Mchezo wa Kandanda**

Sajili ya kandanda ina sura na sifa zake za kipekee zinazoipambanua na kuitofautisha na sajili zingine. Sajili ya kandanda inaweza kubainishwa kuwili kutegemea kama ni kandanda inayotangazwa moja kwa moja kwenye redio na televisheni au ni ile ilioandikwa kama ripoti kwenye magazeti na majarida

- a) Sajili ya kandanda kama zilivyo sajili zingine ina sifa na sura zake ambazo zinaitofautisha na sajili zingine. Iribemwangi na Mukhwana (2010) wanasema lugha ya michezo inaweza kuwa lugha ambayo imeandikwa au lugha ya kuzungumzwa na vile vile wameeleza sifa za michezo kwa ujumla. Sifa za mchezo wa kandanda ni kama zifuatazo;

### **a) Huwa na vichwa**

Habari kuhusu mchezo wa kandanda huandikwa kwa kutanguliza vichwa na kisha taarifa kuhusu mchezo huo kufuata. Vichwa hivi kuhusu habari zitakazofuata pamoja na matokeo ya michezo aghalabu huandikwa kwa herufi kubwa au wino mzito au vyote viwili. Mara nyingi vichwa hivi huonyesha matokeo ya michezo ya timu ambazo zilishiriki katika mechii hizo. Ni kwa misingi hii ambapo endapo timu ya Gor Mahia imeishinda ile ya Tusker kutaandikwa **Gor Mahia 2, Tusker 1 au Wana wa Tusker Walala Miguuni Mwa Gor Mahia au Makucha ya Tusker yashindwa kukwaruza Gor Mahia**, Iribemwangi na Mukhwana (2010:53).

### **b) Kurejelewa kwa taarifa**

Wakati mwingine katika mchezo wa kandanda yaliyopita kuhusu mchezo huo na pia ya wachezaji yanaweza kurejelewa. Mwandishi kwa mfano anaweza kurejelea matokeo ya mchezo uliopita kwa kutaja mabao ambayo yalifungwa na wale ambao

waliyafunga na ulifanyika wapi na tarehe ngapi au siku gani pamoja na mwaka. Vilevile mwandishi anaweza kutaja mahali ambapo mchezo wa timu hizo utafanyika na siku hata kutaja wakati ili wafuasi waweze kuutazama. Aidha, kama maandishi yanahusu mchezo wa kandanda wa Kenya kama vile baina ya Tusker na Gor Mahia, upo uwezekano wa mchezo wa timu zingine za bara za Afrika kurejelewa au hata za Ulaya kama vile mechii baina ya Arsenal na Man City.

**c) Kutengewa kurasa**

Habari kuhusu mchezo wa kandanda katika magazeti na majarida hutengewa kurasa zake maalumu kutegemea gazeti. Hata hivyo habari za michezo zinaweza kuwa kama kichwa cha gazeti ikiwa kumetokea tukio fulani la kushangaza au lisilotarajiwa katika mwanda wa michezo kama vile timu ambayo ni maarufu na ambayo ina wafuasi wengi kufungwa mabao mengi na timu ambayo si maarufu na hata wafuasi wake si wengi. Hizi ni zile za nyuma za magazeti au majarida na pia picha za wachezaji pamoja na vibozo huwekwa ili kusisitiza yale ambayo yameandikwa na mwandishi. Picha hizi na vibozo hunuiwa kutoa na kusawiri hali halisi ilivyokuwa au itakavyokuwa kwa mujibu wa ubashiri au maoni ya mwandishi wa habari husika.

**d) Kila tukio huelezwa**

Wakati wa utangazaji wa mchezo wa kandanda, kila tukio na hatua huweza kuelezwa waziwazi ili wasikilizaji na watazamaji waweze kuelewa kile ambacho kinaendelea uwanjani. Kwa mfano, ikiwa mchezaji wa timu moja akaweza kuumia uwanjani anapoendelea kucheza, lazima tukio hilo liandikwe na mwandishi kwa kutumia msamati unaofaa ili wasomaji waelewe bila ya kukumbwa na matatizo yoyote ya kuufasiri ujumbe huo.

**e) Upanuzi na ubanaji wa maana za maneno**

Katika utangazaji wa mchezo wa kandanda kupitia kwa vyombo vyta ya habari kama vile majarida na magazeti watangazaji wa habari za mchezo wa kandanda kwa njia ya maandishi hupanua na kubana maana za maneno ya kiasili na kwa hivyo kuongeza maana katika lugha inayohusika ili waweze kupitisha ujumbe kwa wasomaji ambao ndio hadhira lengwa.

Sifa na sura hizi zilizotajwa na Iribemwangi na Mukhwaha (2010) zimeweza kufasiriwa nasi huku tukitoa na kuongeza yanayohitajika lakini bila kubadili yaliyomo katika maandishi asilia.

Sajili ya kandanda itadhihirisha sifa hizi za kimazungumzo iwapo wafuasi wa mechii za timu fulani wataenda uwanjani na kuhudhuria mchezo ana kwa ana na vile vile sifa hizi zitadhihirika iwapo wafuasi wa timu fulani kusikiliza matangazo ya mchezo huo kupita kwa vyombo vyahabari kama vile redio, televisheni na *YouTube*. Sifa hizi ni kama zifuatazo:

**f) Upo wingi wa kelele**

Kelele katika mchezo wa kandanda hutokana na wafuasi wengi wa timu zinazoshiriki katika mchezo kuwashangilia wachezaji uwanjani ili kuwatia moyo kwa sababu ya imani kwamba moyo ni kutiana. Iwapo wachezaji wa timu fulani hawachezi vizuri kulingana na matarajio ya mashabiki wao, huenda mashabiki hao wakawakosoa na kwa hivyo kusababisha kelele uwanjani. Sifa hii ya kelele pia inaweza kutokana na muziki unaochezwa kabla ya mchezo kuanza kama vile ngoma ya msondo inayochezwa na wafuasi wa mchezo wa kandanda nchini Kenya.

**g) Matumizi ya muziki**

Mara nydingi matumizi ya muziki katika lugha ya kandanda hudhihirika pale ambapo timu za mataifa mbalimbali zinashiriki katika mechii na kwa hivyo kufanya nyimbo za mataifa za timu hizo kuchezwa kabla na baada ya mchezo huo. Nchini Kenya, mashabiki wa kandanda wana ngoma ya *isukuti*, njuga na vifaa vingine vinogeshavyo muziki kusudi uchezwe. Hii ni njia moja ya kutoa heshima kwa wachezaji na pia kuwatambulisha wachezaji pomoja na wafuasi wao ambao wamehudhuria.

**h) Msamiati maalumu**

Mchezo wa kandanda kimazungumzo kama zilivyo sajili zingine hutumia msamiati wake maalumu kama vile refa, kocha, mpira, washindi, mabao na mlinda lango. Msamiati huu ni mojawapo ya sifa ambazo zinatofautisha sajili ya mchezo wa kandanda na sajili zingine.

**i) Matumizi ya ishara**

Matumizi ya ishara katika mchezo wa kandanda hutokana na refa ambaye ni msimamzi wa mchezo kutumia filimbi kuonyesha mpira kuanza na kumalizika au kuashiria kitendo fulani kimefanyika ili wachezaji wasimamishe mpira. Pia kutumia

ishara fulani kuashiria adhabu fulani kwa wale ambao hawachezi jinsi inavyotakikana.

**j) Utangazaji**

Utangazaji ni sifa ya mchezo wa kandanda na ambao hauzingatii sarufi kwa sababu ya kasi inayokwenda na mchezo wa kandanda. Kuchanganya lugha nyingi pamoja na kuhamisha ndimi kutoka lugha moja hadi nyingine pia hutokea kwa kuwa mtangazaji hana wakati mwingi wa kufikiria maneno ya lugha husika ili aweze kupitisha ujumbe kwa hadhira lengwa na kwa hivyo atatumia maneno ya lugha ambazo anazifahamu. Utangazaji huo hufanywa kupitia kwa vyombo vya habari kama vile redio na televisheni. Vyombo hivi vya habari huweza kunasa na kuhifadhi matangazo hayo ya mchezo wa kandanda katika mtandao wa *YouTube* ili yaweze kusikilizwa baadaye na wasikilizaji.

**k) Matangazo ya biashara**

Matangazo ya biashara ni sifa nyingine ya mchezo wa kandanda kimazungumzo. Mtangazaji anaweza kutangaza bidhaa fulani na bei yake anapoendelea kupeperusha matangazo ya mchezo wa kandanda wa timu husika kwa kuwa wanafikiri ndio wakati unafaa kwa sababu watu wengi wanasikiliza mchezo huo. Kwa mfano, matangazo ya aina ya pombe mpya sokoni kutangazwa kwa kuwa mtangazaji anaamini kuwa wasikilizaji wengi ni wanaume kwa kuwa ndio wanaaminiwa kuupenda mchezo wa kandanda ikilinganshwa na idadi ya wanawake.

**l) Sare**

Wachezaji wa mchezo wa kandanda huwa na sare ambazo zinatofautisha timu moja na nyingine kwa sababu zina rangi tofauti. Hili huwawezesha mashabiki kuitambua timu yao kwa haraka na kuishabikia inapokuwa inacheza uwanjani. Mashabiki nao pia wana sare ambayo inakaribia kufanana na ile sare ya wachezaji wa kandanda na husaidia kutofautisha mashabiki wa timu moja na nyingine. Sare hizi pia ziko na nambari au majina ambayo huwatambulisha wachezaji na jinsi wanavyostahili kucheza.

**m) Kutolewa kwa maoni**

Katika utangazaji wa mpira ulio wa ana kwa ana mashabiki wa mchezo wa kandanda huweza kutuma jumbe fupi kwenye vyombo vya habari kupitia kwa mtangazaji ili

kutoa maoni yao kuhusu timu zinazoshiriki katika mechii. Maoni hayo yanaweza kuwa ni ya kusema ni timu gani itashinda, kwa nini itashinda na hata pia kupongeza wachezaji ambao wanashiriki katika mechii hizo. Mara nyingi mtangazaji husoma maoni hayo na kisha kuendelea na utangazaji wa mchezo wa kandanda wa timu husika.

**n) Upanuzi na ubanaji wa maana za maneno**

Watangazaji wa mchezo wa kandanda kuitia kwa vyombo vya habari kama vile redio na televisheni huwa na sifa ya kupanua na kubana maana za maneno asilia na kwa hivyo kuongeza maana katika lugha husika ili waweze kuitisha ujumbe kwa wasikilizaji au watazamaji ambao ndio hadhira lengwa. Mbinu hii ni bunifu na hutumiwa na watangazaji ili kusisimua wasikilizaji na kuwafanya wavutiwe na utangazaji wao.

Katika visehemu vilivyotangulia tumeeleza na kujadili uhusiano uliopo baina ya lugha na mawasiliano, tumejadili na kufafanua masiala ambayo yanaathiri mawasiliano katika jamii na tumeeleza dhana ya muktadha huku tukitoa maelezo kuhusu muktadha wa hali halisi na muktadha wa kiisumu. Aidha, tumeeleza dhana ya sajili huku tukitoa maoni ya wasomi mbalimbali na sajili ya kandanda na kisha kueleza sifa za sajili ya mchezo wa kandanda. Kisehemu hiki ni msingi wa yale ambayo tumezungumzia katika sehemu ifuatayo katika tasnifu hii.

Mawasiliano yoyote yale, kukiwemo ya kandanda, yana sifa, sheria na kaida zake ambazo huyaongoza. Kwa hali hii, yejote anayechagua sajili fulani ili kuweza kuizungumzia sharti ayafahamu haya. Kwa kuwa utafiti wetu unahu sajili ya kandanda yale tuliyoyasema katika kisehemu cha hapo juu yatatumikizwa katika tasnifu nzima. Kwa misingi hii yale tuliyoyasema katika kisehemu cha hapo juu katika sura hii yatakuwa na manufaa makubwa kwa sura zitakazofuatia kwa kuwa tutayarejelea katika kujibu maswali yetu ya utafiti.

Katika sehemu ifuatayo ya sura hii tumeangazia suala la mfanano na tofauti katika lugha ya kandanda nchini Kenya na Tanzania. Tumelinganisha na kulinganua matumizi ya msamiati katika kubana na kupanua maana za maneno katika mataifa haya mawili kwa kurejelea muktadha wa mchezo wa kandanda.

### **2.3 Lugha na Utangazaji wa Mchezo wa Kandanda**

Kama zilivyo sajili zozote zile, sajili ya mchezo wa kandanda ina lugha yake maalumu inayotumika kuitangazia. Lugha hii ya utangazaji wa mchezo wa kandanda ndiyo tulioishughulikia katika tasnifu hii.

Utangazaji wa mchezo wa kandanda hufanywa kwa kutumia lugha mbalimbali kama vile lugha za kimataifa, kitaifa na lugha za kiasilia ili wasikilizaji ambao ndio hadhira lengwa waweze kupata ule ujumbe ambao unawasilishwa na mtangazaji. Watangazaji wanapotangaza mchezo wa kandanda kwa kutumia lugha hizi, nia yao ni huwa ni kuwawezesha wasikilizaji waweze kuufasiri ule ujumbe ambao wanauwasilisha kulingana na matarajio yao na kwa kufanya hivyo mawasiliano yatakuwa yamefaulu baina yao.

Katika utangazaji wa mchezo wa kandanda kuptitia kwa vyombo vyahabari kama vile redio na televisheni yakiwemo pia magazeti na majarida, kila mtangazaji wa mchezo wa kandanda hutumia lugha kwa njia ya kipekee na ambayo inamtofautisha na mtangazaji mwengine. Kuna wale watangazaji ambao hupanua na kubana maana za maneno ya kiasili na kwa hivyo kuongeza maana katika lugha husika ili waweze kuptisha ujumbe kwa wasikilizaji. Hii ni moja katika mbinu za ubunifu zinazotumiwa na watangazaji ili kusisimua hadhira zao na kuwafanya wasikilizaji au watazamaji kuvutiwa zaidi na utangazaji wao wa kandanda.

### **2.6 LUGHA YA KANDANDA KENYA NA TANZANIA**

Baada ya kuweka misingi ambayo kwayo sura zitakazofuata katika utafiti wetu zitaegemea, katika kisehemu hiki cha sura hii tumelinganisha na kulinganua matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mataifa ya Kenya na Tanzania katika utangazaji wa kandanda. Vipengele vyala lugha ambavyo kwavyo kisehemu hiki kimejikita ni uchanganyaji na uhawilishaji ndimi, matumizi ya mizungu ya lugha, kasi ya utangazaji wa kandanda na lafudhi zinazojitokeza katika utangazaji wa kandanda. Haya matumizi ya lugha yamedhihirisha mfanano na tofauti zilizopo baina ya sajili hii katika nchi hizi mbili.

#### **2.6.1 Uchanganyaji Ndimi**

Kuhusu mbinu hii ambayo inatumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda, Deuchar na Quay (2000) wanaeleza kuwa mbinu hii kwa kawaida hutokea katika jamii ambapo wanajamii wana ujuzi wa lugha zaidi ya moja. Watoto wanaozaliwa katika jamii hii hutumia lugha hizi kwa

sababu watato ambao wana umri mdogo ujuzi wa lugha huongezeka na mabadiliko ya haraka ya lugha kutokea ikilinganishwa kwa watu wakubwa. Wanaendelea kusema kuwa watu waliokomaa pia katika jamii huchanganya ndimi kwa kuwa wana uwezo wa kutumia lugha zaidi ya moja katika mazungumzo kwa njia inayofaa.

Buliba na wengine (2006) na Wamitila (2003) wanasema kuwa uchanganyaji ndimi ni hali ambapo katika usemi kunatokea matumizi ya lugha zaidi ya moja. Maoni yao yanafanana na ya Ipara na Maina (2008) wanaeleza uchanganyaji ndimi kama hali ambapo watu wanapozungumza kwa kutumia lugha fulani uacha kuitumia lugha hiyo na kuanza kutumia lugha nyingine tofauti kwa muda mchache na kisha kurudi katika lugha ya awali.

Richards na wengine (1985) wanaeleza uchanganyaji ndimi kama uingizaji wa maneno ya lugha moja katika matini iliyo katika lugha nyingine. Maelezo yao yanaungwa mkono na Muysken (2000) anayeeleza kuwa uchanganyaji ndimi hutokea katika miktadha mbalimbali wakati ambapo maneno kutoka lugha tofauti tofauti hutokea katika matini moja.

Poplack (1980) anaeleza kuwa kwa kawaida, uchanganyaji ndimi hutokea pale ambapo watumiaji wa lugha huchopeka maneno ya lugha tofauti katika lugha nyingine kwa kuwa wameyasahau au hawajayajua maneno hayo katika lugha ya msingi ambayo inatumika katika mawasiliano.

Berk-Seligson (1986) anasema kuwa uchanganyaji ndimi huonyesha kuwa kuna lugha moja ambayo inatawala lugha nyingine. Kwa mfano, nchini Kenya, lugha ya Kiswahili inaonekana kama yenye inatawaliwa na lugha ya Kiingereza hata baada ya lugha ya Kiswahili kuteuliwa na kuidhinishwa katika katiba ya mwaka 2010 kama lugha rasmi.

Richards na wengine (2008) wanaileza mbinu hii kama uingizaji wa misamiati ya lugha fulani katika usemi ulio katika lugha nyingine tofauti. Katika mchezo wa kandanda nchini Kenya na Tanzania mbinu hii imetumika wakati wa utangazaji wa mpira kwa sababu ya kasi inayokwenda na mpira. Kutokana na kasi ya mpira, mtangazaji hajipati na nafasi ya kufikiri katika lugha moja ili aweze kutangaza katika lugha hiyo hiyo. Kwa hali hii wao hujikuta kwa kuchanganya ndimi kutegemea na ujuzi wa lugha zao. Nchini Kenya ambapo lugha ya Kiingereza husisitizwa, watangazaji hujikuta wakichanganya lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Nchini Tanzania

watangazaji vilevile huchanganya Kiingereza na Kiswahili kuonyesha hadhira zao kwamba wanafahamu vilevile Kiingereza ambalo ni jambo la kujivunia Tanzania.

Imebainika wazi kwamba, utangazaji wa kandanda Kenya na Tanzania hutumia mbinu ya uchanganyaji msimbo. Hata hivyo, watangazaji wa kandanda Kenya huegemea zaidi katika Kiingereza kuliko wale Watanzania ambao nao huegemea zaidi katika Kiswahili. Kwa mfano matumizi ya *lahaula* yatapatikana zaidi Tanzania kuliko Kenya bao linapokaribia kufungwa. Kwa upande mwingine ametumia *force* kufunga *goal* yatapatikana zaidi Kenya. Hii ni kwa sababu taifa la Kenya lilipendelea kutoa elimu kupitia Kiingereza ilhali taifa la Tanzania lilipendelea kutoa elimu kupitia Kiswahili. Mfano;

(1) Ni wakati wa mchezaji wa Tusker kupiga *Penalty* msikilizajii.

Katika tangazo hili neno *penalty* ni la Kiingereza ambalo limepachikwa kwa maneno ya Kiswahili katika utangazaji wa kandanda. Uchanganyaji na hata uhamishaji ndimi kama huu hutokea pale ambapo mchezo unakwenda kwa kasi hivi kwamba mtangazaji hawezi kujikita katika lugha moja pekee. Kutokana na hali hii, lugha anazozifahamu mtangazaji humjia kitabia ili aweze kwenda na kazi ya mchezo huu wa kandanda.

(2) Sofapaka haijaweza kufunga bao lolote katika mechii hii ya leo msikilizaji ni *shame* kubwa kwa wachezaji na mashabiki wa timu hii.

Neno *shame* la Kiingereza limetumika pamoja na maneno ya Kiswahili katika kutangaza mchezo wa kandanda. Katika matumizi haya ya lugha, upo uwezekano kwamba mtangazaji wa kandanda alikosa neno mwafaka la Kiswahili na kwa hiyo akatumia neno *shame* la Kiingereza badala ya neno *aibu* la Kiswahili.

(3) Niyonzima msikilizaji anaonekana kuwa yeye ndio *commander* katika mechii hii ya leo.

Neno la Kiingereza ambalo ni *commander* limepachikwa kwa maneno ya Kiswahili ili kufikisha ujumbe kwa wasikilizaji ambao ndio hadhira lengwa. Neno hili *commander* limetumika kuonyesha ubabe wa mhusika katika mchezo huu wa kandanda.

(4) Azam *football club* wanawalambisha Simba FC mkwaju.

Maneno haya ya Kiingereza ambayo ni *football* na *club* na hata FC yametumika katika kutangazia mchezo wa kandanda. Maneno haya yalitumiwa na mtangazaji pamoja na maneno ya Kiswahili ili kupitisha ujumbe kwa wasikilizaji ambao ndio hadhira lengwa. Isitoshe, Simba FC na Azam FC ndio majina rasmi ya timu hizi za kandanda nchini Tanzania. Hali hii inaonyesha kwamba, majina rasmi ya bidhaa au watu hayafai kutafsriwa bali hutajwa vivyo hivyo.

Inasadifu kwamba mifano mingi ya kuchanganya ndimi inahu su Kiingereza kwa sababu ndicho kinachofundishwa shulenii Afrika Mashariki kukiwemo Kenya na Tanzania mbali na kwamba kitriglosia kinapewa nafasi ya kwanza katika mataifa haya (Abdulaziz 1972). Hata hivyo, kuna mifano mingi ya Kiarabu katika Kiswahili kinachotumika Tanzania zaidi na ilivyo nchini Kenya kutokana na sababu ya utamaduni wa matumizi mengi ya lugha ya Kiswahili nchini Tanzania kama vile ufundishaji na kwa hivyo kulazimika kukopa maneno mengi kutoka kwa lugha ya Kiarabu.

### **2.6.2 Uhawilishaji wa Msimbo**

Hii mbinu vilevile hutumika katika utangazaji wa mchezo wa kandanda. Kuhusu mbinu hii, Habwe na wengine (2010) wanaeleza kuwa uhawilishaji msimbo hutokea wakati ambapo mtu ambaye ana ujuzi wa lugha zaidi ya moja anazitumia kwa kubadilishana nafasi.

Buliba na wengine (2006) wanaeleza kuwa uhawilishaji wa msimbo ni hali ambayo hutokea wakati mtumiaji wa lugha ambaye ana umilisi wa lugha nyingi anabadilisha usemi wake kutoka lugha moja na kuanza kuitumia lugha nyingine. Wanaeleza kuwa uhawilishaji wa msimbo huu hutegemea mtindo, kichwa cha kile kinachozungumziwa, wasikilizaji na eneo la mazungumzo. Wanatoa mfano wa watoto wa Kihispaniola ambao wanahawilisha msimbo wanapozungumza na walimu kutoka Kihispaniola hadi Kiingereza. Mfano huu unaashiria kuwa ubadilishaji wa eneo la mazungumzo ni mojawapo ya sababu za uhawilishaji msimbo.

Hymes (1974) anaeleza kuwa uhawilishaji wa msimbo ni hali ambapo kuna matumizi ya sentensi mbili au zaidi ambazo ni za lugha mbili tofauti na hata pia zenyé mitindo na sheria tofauti ya lugha zinatokea pamoja katika mazungumzo. Kila sentensi huwa na maana yake ambayo inajisimamia na vilevile huzingatia kanuni na sheria za utunzi ambazo zinakubalika katika lugha husika.

Gumperz (1982) na Appel na Muysken (1987) wanaeleza kuwa watangazaji wa kandanda wanahawilisha msimbo wakiwa na malengo fulani ambayo wanataka kuyatimiza kwa hivyo hawajikuti wakihawilisha msimbo ovyo ovyo. Wanaendelea kusema kuwa baadhi ya malengo ambayo wanataka kutimiza ni kama vile kufurahisha hadhira, kuelezea zaidi jambo fulani, kuweka mkazo na hata kujitambulisha.

Watangazaji wa kandanda hujikuta wameruka kutoka lugha moja hadi nyingine wanapokuwa wanatangaza kandanda. Hali hii ndiyo inayojulikana kama uhawilishaji wa msimbo. Katika utangazaji wa kandanda Kenya na Tanzania watangazaji hujikuta katika hali ya kutangaza katika lugha ya pili kwa sababu mbalimbali. Mara nyingi hali hii hutokea kutoka Kiswahili hadi Kiingereza, Kiarabu na hata lugha za kiasili. Vilevile, mashabiki wanaopewa fursa ya kutoa maoni yao na watangazaji mpira unapoendelea, unapokuwa mapumzikoni au unapotamatika huweza kuhawilisha msimbo kutoka lugha msingi ya Kiswahili hadi lugha zao za kiasili. Hali hizi zote huchochewa na hisia za wahusika. Kwa mfano, nchini Kenya mashabiki wa timu ya Gor Mahia watasema *maber ainya* wanapoulizwa kama wameuona aje mpira ulivyokwenda na mtangazaji wa kandanda kwa lugha ya Kiswahili.

Kiulinganishi, utafiti wetu umebaini kwamba uhawilishi wa msimbo katika utangazaji wa kandanda hufanyika zaidi katika nchi ya Kenya kuliko ilivyo Tanzania. Sababu ya hali hii inaweza kukisiwa kuwa katika suala la sera ya lugha, katika elimu na upangaji lugha katika nchi hizi mbili za Afrika Mashariki. Mfano;

(5)     *Balama Mapinduzi anaupiga mpira, go-o-l! What a fantastic goal!*

Katika mfano huu, mtangazaji alihama kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kiingereza kuonyesha bao lililofungwa na mchezaji Balama Mapinduzi.

(6)     *Mchezo unakaribia kumalizika bado Simba in control.*

Mtangazaji alihama kutoka kwa lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kiingereza katika matangazo ya mechi ya Simba na timu pinzani. Timu ya Simba ilikuwa imefunga mabao mengi ikilinganishwa na ile walikuwa wanapinzana nayo.

(7)     *Onyango anapiga ndefu na kufunga bao hilo bila tatizo lolote. Right time, right position, right thing he has done. Bravo! Bravo! My brother.*

Mfano huu wa uhamishaji wa ndimi ulitokana na matangazo ya kandanda kwenye mtandao wa *YouTube* nchini Kenya mnamo mwaka wa 2019. Mtangazaji anapongeza mchezaji ambaye ameifungia timu bao na kwa hivyo kuhamisha ndimi kutoka kwa Kiswahili hadi Kiingereza.

Leksimu ya Kiingereza *fly* imeongezea viambishai vya awali vya Kiswahili na kutumiwa na mtangazaji kutangazia kandanda.

(8)     Bernard Morrison anamwekea Harun Niyonzima, Baba Haruna  
*anacontrol* mpira ule usitoke katika eneo la hatari.

Neno *control* la Kiingereza limetumika katika kutangazia kandanda baada ya kuongezewa viambishi awali vya Kiswahili.

Mifano ya aina hii ya matumizi ya lugha ilipatikana kwa wingi nchini Tanzania kuliko ilivyo nchini Kenya ambapo neno moja tu kucontrol lililojitekeza wazi.

Hata hivyo, ingawa kwetu hali hii inaonekana kama ya uhawilishaji ndimi kwa watafiti wengine itaonekana kuwa ni uchanganyaji wa ndimi (mrejelee Myers-Scotton 1997).

### **2.6.3 Nafasi ya lafudhi katika Utangazaji**

Lafudhi ni upekee wa mtu au watu wa kutamka sauti zinazowadhihirisha wao kama wao na kuwatofautisha na wengine wasiokuwa wao. Kwa hali hii, dhana ya lafudhi inahusu *usisi* dhidi ya *uwao*. Katika utangazaji wa kandanda kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili hali hii iimeweza kujitokeza na kuwatofautisha watangazaji na hata mashabiki walio Wakenya na Watanzania. Hali hii vilevile imejitokeza kutofautisha watangazaji na mashabiki wanaotoka pwani na bara ya Kenya na Tanzania. Vilevile viwango vya elimu vya watangazaji vimeweza kujitokeza kama kigezo muhimu cha kutofautisha lafudhi za watangazaji wa kandanda katika mataifa ya Kenya na Tanzania.

Tukianza na kigezo cha utaifa ilibainika wazi kwamba pale ambapo Wakenya wanatumia sauti /l/ katika utangazaji wao Watanzania wanatumia sauti /r/ katika utangazaji wao. Hata hivyo lafudhi hii ilijitokeza kimatamshi na wala si kimaandishi maana ilipokuja katika ripoti za kandanda zilizoandikwa sauti iliyotumika ilikuwa ni /l/. Hali hii inadhihirisha wazo kuwa lafudhi hujidhihirisha sana kimazungumzo kuliko kimaandishi.

Mashabiki wa kandanda kutoka Kenya na Tanzania walidhihirisha tofauti za kitaifa kwa namna walivyotamka maneno ya mchezo wa kandanda. Neno *lala* la Kiswahili lilitamkwa kwa matumizi ya sauti ile ile /l/ ya Kiswahili lakini kulidhihirika tofauti baina ya mashabiki wa kandanda nchini Kenya na Tanzania. Hali hii inaonyesha wazi kwamba kuna tofauti za kilafudhi katika lugha ile ile moja ya Kiswahili kama ilivyo kwa Kiingereza. Tofauti hii ni ya kimaeneo kinyume na Kiingereza kinachoonyesha tofauti ya kitabaka na kijiografia.

Ilibainika kuwa watangazaji walioajiriwa kutokana na kufuzu kwao katika Kiswahili walikuwa na athari ndogo sana hasa kilafudhi kwa Kiswahili sanifu katika utangazaji wao wa kandanda ikilinganishwa na wale walioajiriwa kwa sababu ya uzoefu wao wa kuzungumza Kiswahili. Kwa mfano, katika utamkaji wa siku Alhamisi mtangazaji kutoka Kenya alitamka kama Alkhmisi kwa sababu ya lafudhi yake ya Pwani. Vivyo hivyo, kutegemea kama mtangazaji alitokea pwani au bara ya Kenya au Tanzania alikuwa na athari nyingi za Kiswahili chenye misingi ya Kiarabu kutokana na maeneo ya pwani kuishikilia dini ya Kiisilamu inayonkuu vifungu kutoka kuruhani kwa Kiarabu kimatamshi kuliko wale wa bara waliofunzwa Kiswahili sanifu skuli. Mfano;

- (9) Kalibu sana msikilizaji katika uwanja wa Benjamin Mkapa ili tuweze Kutazama mechii ya leo, ni mechii baina ya vigogo wa jadi, Yanga na Simba.

Nchini Tanzania sauti /l/ inatumika badala ya /r/ na wakati mwengine sauti hizi zikatumika kama zinazoweza kubadilishana nafasi kama ilivyo katika *kipengere* na *kipengele*.

- (10) Wanayanga wamerarishwa chini na Wanasimba msikilizaji baada ya kuwafunga goli moja kwa sufuri.

Katika mfano huu badala ya kusema *lala* mtangazaji ametamka kama *rara*.

- (11) Leo msikilizaji wanasofapaka wamelala miguuni mwa wanatusker baada ya kushindwa kufunga bao. Hawaamini walichokiona.

- (12) Msikilizaji ni fursa nzuri nakukaribisha katika uwanja wa Kasarani Kushuhudia mechii baina ya Gor Mahia na FC Leopards.

Kama inavyoonekana kutokana na mifano hii miwili, watangazaji wa kandanda Kenya hawazungumzi kwa Kiswahili kilichojaa lafudhi isiyo sanifu na hali hii inaweza labda kuelezwaa

kwa kuzingatia masiala kama vile sera ya uajiri katika vyombo vya habari na viwango vya matamshi vya waajiriwa hawa katika utangazaji.

#### **2.6.4 Matumizi ya Mizungu ya Lugha**

Mizungu ya lugha ni matumizi ya lugha isiyo ya moja kwa moja hivi kwamba ili kupata maana lengwa sharti mhusika atumikize macho ya ndani pamoja na tajriba zake za maisha. Wamitila (2003) anaeleza kuwa mizungu ya lugha ni mafungu ya maneno yenye maana ambayo imefichika. Mizungu ya lugha huendana na mafumbo, jazanda, ndumo na mbinu zingine anuai za mawasiliano yasiyo ya moja kwa moja.

Matumizi ya mizungu ya lugha inahusishwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda nchini Kenya na Tanzania.

##### **2.6.4.1 Matumizi ya Methali**

Wamitila (2004) anaeleza kuwa methali ni fungu la maneno linalotumiwa na jamii ya watu kwa namna maalum inayotoa maadili na ambalo ni la kimapokeo na linaundwa kwa njia maalum, lina lengo mahsususi, lina lengo la kuongoza, kuonya, na kukashifu. Maoni haya yanafanana na Ngure (2003) ambaye anaeleza kuwa methali ni semi fupi ambazo zinakubalika na kutumika katika jamii na maana yake ni fiche na hutumika kueleza falsafa na ukweli wa jamii inayohusika.

Methali ni tungo katika lugha ambazo hutoa nasaha na mafunzo kwa umma na ambazo mara nyingi huwa katika vipande viwili vyenye kujengana ili kukamilisha maana iliyofumbwa. Kwa mfano katika mchezo wa kandanda timu inapokuwa nyumbani mara nyingi mtangazaji husema *mcheza kwao hutuzwa au mcheza kwao hutunzwa* kwa maana kwamba lazima ashabikiwe na hata kushinda. Watangazaji wa kandanda nchini Kenya na Tanzania hutumia methali kama njia mojawapo ya utangazaji wa kandanda. Mfano;

(13) *Mbiu wa mgambo ukilia kuna jambo.* Ni mechii kubwa msikilizaji Gor Mahia dhidi ya Sofapaka nchini Kenya katika uwanja wa Kasarani.

Katika mfano huu, methali mbiu wa mgambo ukilia kuna jambo imetumika na mtangazaji wa kandanda kwa maana kuwa mashabiki wa timu maarufu wamejitokeza ili waweze kushangilia timu yao. Ujitokezaji huu wa mashabiki ni ishara tosha kuwa mchezo wa kandanda utacheza na ndio maana wanalinganishwa na mbiu wa mgambo.

(14) Msikilizaji ni ndani ya uwanja wa Kasarani jijini Nairobi ambapo mechii baina ya AFC Leopards na Gor Mahia inakaribia kuanza. *Leo ni leo msema kesho ni mwongo* msikilizaji.

Methali hii imetumika kuashiria kwamba mechii hii itachezwa leo liwe liwalo na kwa hiyo mshindi atabainika wazi timu hizi zitakapochuana leo hii.

(15) Msikilizaji nakukaribisha katika mechii inayoanza baina ya Yanga na Simba usije ukachelewa kuungana nami kwani *chelewa chelewa utapata mwana si wako*.

Mtangazaji wa kandanda ametumia methali hii kwa maana ya kuwasihii mashabiki wafike mapema wasije wakajilaumu kwa kukosa uhondo kuhusu mechii baina ya timu ya Yanga na Simba.

(16) Ni mechii kati ya Simba na Azamu msikilizaji. Timu hizi zimekuwa zikijitayarisha juma nzima kila moja ikitaka kuipuka mshindi katika mechii ya leo Kweli *mtaka cha mvunguni sharti ainame*.

Methali hii ya mtaka cha mvunguni sharti ainame ni methali ambayo imetumika na mtangazaji wa kandanda kwa maana kuwa ukitaka kufaulu katika chochote lazima utie bidi.

#### **2.6.4.2 Takriri**

Dhana ya takriri hutumika katika mawasiliano kumaanisha usisitishaji au ukariri wa jambo fulani. Lengo la takriri huwa ni kutilia mkazo kile kinachosemwa au kinachotukia. Kulingana na Wamitila (2003) katika mbinu ya takriri kuna urudiaji wa mistari, virai, vishazi, neno na hata sauti na kwa hivyo kunatokea aina za takriri.

Kwa mujibu wa Briely (1985) mbinu ya takriri hutumiwa ili kutia mkazo na kueleza kwa kina ujumbe unaowasilishwa kwa hadhira. Katika utangazaji wa kandanda Kenya na Tanzania takriri hutumika pale ambapo mchezaji analifanya jambo tena na tena au anamtia mtangazaji na

msikilizaji katika hali ya taharuki kwa kutojua kama tokeo litakuwa lipi. Kwa hali hii bao linapokaribia kufungwa, mtangazaji atasikika akisema *go-o-o-li*. Mfano;

- (17) Ateyo anaimimina ndani katika nafasi ...*g-o-o-l!* Huwezi kuamini kinachotokea msikilizaj. Anaicharaza! Anaicharaza! Anaicharaza! Simba wanashangaa.

Mtangazaji wa kandanda anarudia neno *charaza* kuonyesha namna timu ya Simba imewza kufungwa mabao mengi na timu pinzani.

- (18) Balama Mapinduzi, Balama! Balama Mapinduzi anaupiga mpira, Whata a shoot! Anauzokemeza mpira kwenye Kamba Mapinduzi. Anautandika kweli kweli Balama Mapinduzi.

Katika kukariri jina la mchezaji huyu husika mtangazaji anaashiria bidii anayotia yeye katika kukaragaza mpira akiwa uwanjani.

- (19) Katikati mwa uwanja, stephene Ochola, Ochola anaachilia kule kwake Brian, Brian ananyang'anywa ule mpira, mpira unatoka nje.

Majina ya wachezaji yanarudiwa na mtangazaji wa kandanda kuonyesha jinsi wanavyocheza kandanda uwanjani.

- (20) Otieno anakimbia na mpira, anakimbia na mpira msikilizaji, Otieno anauelekeza kwa Vincent, mpira unakuwa mwangi na kutoka nje.

Jina la mchezaji limekaririwa katika mfano wa hapo juu na mtangazaji wa kandanda ili kuonyesha bidii aliyo nayo mchezaji huyo uwanjani katika kucheza kandanda.

#### **2.6.4.3 Tashbihi**

Hii ni mbinu ya ulinganishi wa vitu viwili na iliyio ya moja kwa moja. Kulingana na Chapman (1989) katika mbinu ya tashbihi vitu vinavyolininganishwa huwa na ushabihiano. Anaendelea kusema kuwa katika mbinu ya takriri vitu viwili ambavyo hurejelewa huwa na tabia inayolingana. Maoni haya yanafanana na ya Lucas (1955) ambaye anaeleza kwamba mbinu hii ya tashbihi hutumiwa ili kuweka fikira mbili zinazoeleza jambo fulani kuwa sambamba.

Mbinu hii inatumika katika utangazaji wa mchezo wa kandanda kusema jinsi timu, wachezaji, mashabiki na hata refa walivyo kwa kutumia vifananishi kama vile, kama, mfano, ja n.k. Mbinu hii imetumika katika utangazaji wa kandanda Kenya na Tanzania ambapo timu zimeweza kudokezwa kulingana na uwezo wao. Kwa mfano, nchini Kenya, utafiti wetu ulionyesha kuwa mtangazaji aliuliza kama timu ya Mathare United ina makucha kama ya AFC Leopards (chui). Mifano ifuatayo na ambayo imetokana na utafiti wetu inafafanua matumizi haya ya lugha katika kandanda zaidi.

(21) Leopards wanawafunga mabao matatu timu ya Tusker na *kuwadharau kama ukuni wa kiangazi*.

Mfano huu wa tashbihi ulitumika na mtangazaji wa kandanda kuonyesha namna wachezaji wa Leopards waliwaona wachezaji wa Tusker kuwa hawafai baada ya kuwafunga magoli mengi. Wanawadharau namna ukuni wa kiangazi unavyodharauliwa katika kuwashia moto.

(22) Mchezo unakamilika na Sofapaka msikilizaji imepokea *kichapo kama cha kelbu msikitini* kutoka kwa Gor Mahia.

Timu ya Sofapaka imechapwa magoli mengi na Gor Mahia. Mtangazaji kwa hivyo ameweza kufananisha kichapo hicho na kichapo cha kelbu msikitini.

(23) Kagere anaifungia Yanga goli na *kutetema mithili ya tembo ndani ya mbuga*.

Mtangazaji wa kandanda ametumia mbinu hii katika mfano wa hapo juu kuonyesha kutetema kwa furaha aliyokuwa nayo Kagere baada ya kufungia timu ya Yanga bao. Furaha hiyo inafananishwa na ya tembo akiwa ndani ya mbuga.

(24) Hivi sasa kila kitu kiko tayari katika uwanja wa Benjamin Mkapa Nikukaribishe sana katika *siku inayopendeza mithili ya msichana mrembo*.

Mtangazaji anafananisha siku ambayo mechii itakapochezwa na jinsi msichana mrembo anavyopendeza.

#### **2.6.4.4 Tashhisi**

Kulingana na Njogu na Chimerah (1999) katika mbinu ya tashhisi vitu visivyo na uhai hupewa sifa za vitu vilivyo na uhai kama vile kutazama, kutembea, kula na kadhalika. Maelezo yake yanaungwa mkono na Wamitila (2003) ambaye anasema kuwa katika mbinu ya tashhisi vitu visivyo na uhai hupewa uwezo wa kutenda mambo jinsi vitu vilivyo na uhai vinavyotenda.

Huu ni uhuisishaji wa vitu au kuvipa vitu sifa ambazo ni za vitu vingine lakini kutokana na mfanano wa uhuisishaji au uelekezaji wa vitu hivyo husika. Kutokana na utafiti wetu tulipata kwamba timu za kandanda kama vile Simba ya Tanzania na AFC Leopards (Chui) ya Kenya ziliambatishwa na makali yanayokwenda na wanyama hawa. Mbali na haya, mifano ifuatayo tulioipata kutokana na utafiti wetu inadhihirisha matumizi haya katika utangazaji wa kandanda nchini Kenya na Tanzania.

(25) Gor Mahia wamefunga timu ya Tusker mabao mengi msikilizaji mpaka nyavu za wanatusker zinatemeka.

Sifa ya viumbe vyenye uhai ya kutetemeka kwa sababu ya hisia fulani imepewa nyavu na mtangazaji wa kandanda kuonyesha namna mabao mengi yamefungwa na timu ya Gor Mahia huku Tusker ikiwa haijafunga bao.

(26) Otieno anapiga ndefu msikilizaji, *mpira unakuwa mwingi na kutoka nje.*

Mpira umepewa sifa ya viumbe vyenye huai ya kuweza kukimbia au kutembea na kutoka nje. Hii ni baada ya Otieno kupiga mpira nje ya uwanja kunakochezewa mechii.

(27) Yanga inaongoza kwa mabao 4 na Azamu 2 hapa msikilizaji ni karamu ya magoli *milango inatisika kwa raha zake.*

Katika mfano huu, milango imepewa sifa ya viumbe vyenye uhai ya kuwa na raha kuashiria namna timu zote mbili husika zimeweza kufunga mabao mengi.

(28) Mcbezaji wa Yanga anapiga mkwaju wa *penalty* msikilizaji na kufunga bao. Watoto wa mtaani wanasema kuwa ile *nyavu imeitikia bao hilo.*

Sifa ya binadamu ya kuitikia au kulikubali jambo au wazo fulani imepatiwa nyavu baada ya goli kufungwa na mtangazaji wa kandanda.

#### **2.6.4.5 Misemo**

Wamitila (2003) anaeleza misemo kama vifungu vya maneno ambavyo huweza kutumiwa kuonyesha maana fulani ambayo inaweza kutofautiana na maana asilia ya vifungu hivyo. Anaendelea kusema kuwa, vifungu hivyo huwa na muundo fulani aghalabu usiobadilika japo maana zenyewe za vifungu hivyo huweza kubadilika na kupanuliwa kimaana. Mbinu hii inatumika katika utangazaji wa mchezo wa kandanda kama inavyodhihirika hapo chini.

- (29) Otieno wa Gor Mahia ni mchezaji mzuri ambaye *anamezewa mate* na timu nyangi.

Msemo *mezea mate* umetumiwa katika utangazaji wa kandanda kwa maana ya mchezaji mzuri ambaye anatamaniwa na timu nyangi.

- (30) Ni dakika themanini na tano msikilizaji mchezo uko karibu kumalizika lango la Wazito FC linaendelea *kulala njaa* huku Tusker wakiwa na mabao mawili.

Katika mfano wa hapo juu, msemo *lala njaa* ambaeo una maana ya kulala usiku bila kutia chakula tumboni limetumika katika mchezo wa kandanda kwa maana ya Wazito FC haijaweza kufunga bao lolote.

- (31) David juma msikilizaji *akapiga mbizi* kuangalia akapata ni nyasi pekee yake lakini chuma kile kiko ndani ya wavu.

Msemo *piga mbizi* wenge maana ya kuogelea majini umetumiwa na mtangazaji wa kandanda kwa maana ya kupiga mpira.

- (32) Simba FC *inatiwa mkononi* na Yanga kwa kulimwa mabao 3-0.

Mtangazaji wa kandanda ametumia msemo *tia mkononi* wenge maana wa kukamata kitu au kushika kitu mkononi kuonyesha namna timu ya Simba imeweza kufungwa mabao mengi na timu ya Yanga.

#### **2.6.4.6 Maswali ya Balagha**

Leech (1983) anaeleza kwamba maswali ya balagha ni semi ambazo zinatia hamu mawazo fulani na kuzua matokeo pamoja na mazoea kwa mpokezi wa ujumbe.

Habwe (1999) anaeleza kuwa maswali ya balagha huweza kuhitaji majibu kwa kuwa yanaonekana kuvutia kwa kiwango cha juu kama yana pengo la habari. Anaendelea kusema kuwa maswali ya balagha hutumiwa na mtoaji ujumbe ili kuwafanya wasikilizaji waweze kufikiria zaidi.

Haya ni maswali ambayo katika mazungumzo ya kawaida huwa hayana majibu kwa sababu majibu yanajulikana na umma au hadhira lengwa. Hali hii vilevile hujitokeza katika mchezo wa kandanda nchini Kenya na Tanzania. Kwa mfano timu ya Yanga FC inapocheza na timu ndogondogo kama vile Kigoma United na mtangazaji aulize kama ushabiki mkubwa utatoka wapi. Haitaji jibu ila kunyamaziwa kwa kuwa Yanga FC ina ufuasi mkubwa nchini Tanzania. Ifuatayo ni mifano tulioipata kutokana na utafiti wetu kuhusu utangazaji wa kandanda nchini Kenya na Tanzania.

(33) G-o-o-l! Goli gani hili linafungwa katika uwanja wa Benjmini Mkapa?

Msikilizaji ulikuwa unategemea goli kama hili lifungwe na Magere mapema mapema mwanzoni mwa ligi magoli matamu matamu kiasi hiki? Ulitegemea jambo kama hili alifanye Magere?

Mtangazaji wa kandanda ametumia swali hili ili wasikilizaji ambao ndio hadhira lengwa waweze kujiwazia na vilevile kuteka hisia ya wasikilzaji.

(34) Kipi kinakushangaza, Yanga kutokea nyuma au Fahim Salimu kufanya kile ambacho mara zote huwa anafanya? Mbona mambo ni ya kikubwa sana? Nani alimpa jina la Fahim Toto msikilizaji?

Katika mfano huu, mtangazaji wa kandanda anatumia maswali ya balagha ambayo haitaji majibu kutoka kwa wasikilizaji ambao ndio hadhira lengwa ili kuonyesha namna mchezaji Fahim Salimu ana uwezo wa kufunga mabao kila wakati anapoichezea timu yake na kila mmoja wa wasikilizaji wa kandanda analifahamu hilo.

(35) Msikilizaji ni dakika hamsini na tano na timu ya Sofapaka inafungwa bao la nne na Gor Mahia. Nini kilifanyikia timu ya Sofapaka? Sisemi kitu!

Swali la balagha katika mfano wa hapo juu limetumiwa na mtangazaji wa kandanda kuonyesha namna uchezaji wa timu ya Sofapaka haupendezi kama vile mwanzoni ulivyokuwa unapendeza kwani hawana uwezo wa kufunga bao hata moja.

(36) Ni mechii kati ya timu ya Tusker na Ingwe msikilizaji. Ni gani itashinda katika siku ya leo?

Mtangazaji amelitumia swali la balagha katika mfano wa hapo juu katika utangazaji wa kandanda ili wasikilizaji ambao ndio hadhira lengwa waweze kuijwazia wao wenyewe na kubaini ni timu gani itashinda baina ya timu mbili husika.

Utafiti wetu haukuweza kubaini wazi kama maswali ya balagha hutumika kwingi au kwa uchache nchini Kenya au Tanzania kwa sababu hili halikuwa moja katika malengo yetu makuu katika utafiti wetu. Labda kama pendekezo utafiti zaidi kuhusu hali hii unaweza kufanywa ili kubaini hili.

## **2.5 HITIMISHO**

Katika sura hii tumelinganisha na kulinganua vipengele mbalimbali vya utangazaji wa mpira wa kandanda nchini Kenya na Tanzania. Haya yote tumeyafanya baada ya kutia msingi wa kile kinachotarajiwu katika sajili ya kandanda. Imejibainisha kuwa kuna tofauti na mfanano wa hapa na pale wa kimazungumzo na kimaandishi.

Katika sura ifuatayo ya utafiti hu tumeliangalia suala la mabadiliko ya kisemantiki katika utangazaji wa kandanda nchini Kenya na Tanzania kwa kurejelea lugha ya Kiswahili.

## **SURA YA TATU**

### **3.0 UPANUZI NA UBANAJI WA MAANA NCHINI KENYA NA TANZANIA**

#### **3.1 Utangulizi**

Katika sura ya pili tumepitia kwa jumla dhana ya sajili huku tukirejelea mchezo wa kandanda katika ujumla wake. Vilevile tumeweza kulinganisha na kulinganua matumizi ya lugha ya kandanda katika mataifa ya Kenya na Tanzania na kuweza kuhitimisha kwamba kwa ujumla watangazaji wa kandanda Tanzania wanayo makini kubwa ikilinganishwa na wenzao wa Kenya.

Katika sura hii ya tatu tumeshughulikia ubanaji na upanuzi wa maana katika lugha ya kandanda nchini Kenya na Tanzania. Upanuzi na ubanaji wa maana huweza kujitokeza katika miktadha mbalimbali ya matumizi ya lugha. Katika sura hii, lengo letu kuu ni kubainisha mabadiliko ya kisemantiki yaliyotokea katika mchezo wa kandanda nchini Kenya na Tanzania kwa kuzingatia upanuzi na ubanaji wa maana. Kwa kufanya hivi tumeweza kubaini ikiwa kuna matumizi mengi ya upanuzi wa maana kuliko yale ya ubanaji wa maana ili kuweza kutahadharisha walengwa katika utangazaji wa kandanda dhidi ya kuchukulia maana za maneno kijuu juu. Vilevile kwa kufafanua upanuzi na ubanaji wa maana katika mchezo wa kandanda nchini Kenya na Tanzania tutaweza kuwarahisishia uelewa wa maneno watazamaji, wasikilizaji na wasomaji wa lugha ya mchezo wa kandanda.


#### **3.2 Michakato ya Upanuzi na Ubanaji wa Maana katika Kandanda**

Vipengele vya upanuzi na ubanaji wa maana katika mchezo wa kandanda ambavyo tumeshughulikia ni hivi vifuatavyo:

##### **3.2.1 Ubanaji wa maana kileksika**

Mchakato huu wa ubanaji wa maana za maneno hutokea wakati ambapo maana nyingi za neno iliyosimbwa kisemantiki hufinywa na maana moja kuwasilishwa kwenye muktadha wa mazungumzo na kusababisha zile maana zingine kubanwa, kusauhulika na hata kupotea kabisa.

Katika mchoro ufuatao, tunaona kuwa dhana inayowasilishwa ni finyu kuliko dhana iliyosimbwa kisemantiki kwenye tamko. Hii inalazimisha msikilizaji kufanya mchakato huu wa ubanaji na kuzingatia muktadha wa mazungumzo ili aweze kuelewa dhana finyu inayowasilishwa na ambayo ni kijisehemu cha dhana pana iliyosimbwa kwenye tamko hilo.



*Chanzo: Wilson (2003:7)*

Ifuatayo ni mifano michache ya ubanaji iliyojitokeza katika data tulioikusanya kuhusiana na mchezo wa kandanda nchini Kenya na Tanzania huku tukijiegemeza katika matangazo ya mchezo.

(38) Otieno wakati anaweka ile *kinga* ukiangalia msikilizaji mpira ukiwa kwenye mstari aliugusa na kutoka nje.

Neno *kinga* ni wazi na la kijumla kwa sababu neno hili lina maana nyingi kama vile zuia madhara fulani yasifike kwa mtu au mahali, tayarisha bindo, mkono au chombo ili kupokea kitu, jambo au dawa ya kujiepusha na madhara, kipande cha ukuni kinachowaka, chenye moto au kinachoungua. Katika muktadha huu wa utangazaji wa mchezo wa kandanda neno hili *kinga* limetumika kuwasilisha maana moja ambayo ni zuia madhara fulani yasifike kwa mtu au mahali na maana zingine za neno hili zinafungiwa nje kama vile tayarisha bindo au mkono au chombo ili kupokea kitu jambo au dawa ya kujiepusha na madhara, kipande cha ukuni kinachowaka, chenye moto au kinachoungua. Kimsingi *kinga* inayozungumziwa katika mfano uliopo hapo juu ni ile ya kuzuia mpira kufungwa katika lango la timu ya Otieno.

(37) Msikilizaji mpira unatoka *nje*, mpira unarudishwa *ndani* na Ditram Nchimbi wa Yanga FC, Mpira unaanza tena msikilizaji huku Yanga FC wakiwa na bao moja huku Simba FC wakiwa hawajafunga bao lolote msikilizaji.

Neno *ndani* katika lugha ya Kiswahili limesimba dhana NDANI. Dhana iliyosimbwa kwenye neno ndani ni wazi na ya kijumla kwa kuwa inajumuisha kitu chochote au sehemu yoyote ambayo imefunikwa. Ili msikilizaji aweze kupata maana finyu ambayo imesimbwa na neno hili anastahili kuzingatia muktadha wa matumizi ya neno ndani ili aweze kuelewa maana ambayo


inakusudiwa na mtangazaji. Kutokana na huu wakati mahususi wa mchezo wa kandanda msikilizaji anafasiri dhana ya neno ndani kuwa uwanjani na kwa hivyo kuchukua mwelekeo wa maana ya sehemu yoyote iliyofungwa na wala si ndani ya kitu kingine. Kwa upande mwingine, matumizi ya *nje* yana maana ya kinyume cha ndani. Katika muktadha wa mchezo wa kandanda lina maana ya kutokuwa uwanjani maana mpira huchezewa ndani ya uwanja.

Baada ya kutoa mifano hii miwili ya ubanaji wa maana katika mchezo wa kandanda ifuatayo ni mifano kuhusu upanuzi wa maana kileksika katika utangazaji wa kandanda kama ulivyojitokeza nchini Kenya na Tanzania.

### 3.2.2 Upanuzi wa Maana Kileksika

Upanuzi wa maana kileksika ni hali ambapo neno ambalo lina maana moja katika hali ya kawaida linaongezewa maana ya ziada na hivyo kufanya matumizi ya neno hilo kuwa pana ikilinganishwa na ile ambayo imesimbwa kisemantiki. Blutner (2011) anatoa mfano wa kitenzi ‘ona’ huku akimrejelea Swetser (1990). Anasema kitenzi ona chenye maana ya kutazama kwa kutumia macho maana yake inaweza kupanuliwa zaidi na kumaanisha picha anayokuwa nayo akilini wakati wa mazungumzo kumaanisha kujua kitu mtu alitarajia kusema au kujua mwelekeo wa mtu hata kama hajausema yeeye mwenyewe.

Kielelezo kilichopo hapa chini ni cha upanuzi wa maana kwa mujibu wa Wilson (2003:07).



*Chanzo: Wilson (2003:7)*

Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya upanuzi wa maana kileksika iliyotokana na data tuliyokusanya kuhusiana na mchezo wa kandanda nchini Kenya na Tanzania.

- (38) FC Leopards ilinyamazisha *mabwenyenye* Tusker mabao 2-0 katika mech  
ya 18.

Katika mfano huu kumetumiwa neno *mabwenyenye* na vilevile *kunyamazisha*. Katika hali ya kawaida mabwenyenye ni matajiri wa kupindukia. Katika mfano huu, timu ya Tusker ambayo inamilikiwa na wagema wa *East Afrika Breweries* inalinganishwa na matajiri wa kupindukia kutokana na biashara yao ya pombe. Kutokana na historia ya kabla ya mchuano unaotangazwa au kuzungumziwa, timu ya Tusker imekuwa ikishinda mechizake na hiyo ni sababu mojawapo ya wao kuitwa *mabwenyenye*. Katika hali hizi zote kumetokea upanuzi wa maana kileksika. Vivyo hivyo, katika mfano huu, neno *kunyamazisha* lina maana ya kumfanya mtu awe kimya lakini lilivyotumika hapa sivyo. Hapa neno hili limetumika kwa maana ya kufungwa na kwa hiyo kumekuwa na upanuzi wa maana kileksika.

(39) Yanga FC *imelima* Azamu FC mabao 3-0.

Neno *kulima* ni nomino inayotokana na kitenzi lima. Nomino hii ina maana ya kuchimbua ardhi hasa shambani kwa matayarisho ya upanzi. Hata hivyo neno hili limetumika katika mchezo wa kandanda nchini Tanzania kumaanisha kwamba timu ya Yanga imeishinda timu ya Azamu kwa namna ambayo haikutegemewa. Ili kutupa picha halisi ya hali ilivyokuwa, neno *kulima* lilitumika na huu ni upanuzi wa maana kileksika.

### **3.2.3 Upanuzi wa kisitiari**

Wataalamu mbalimbali wamezungumzia suala hili la upanuzi wa kisitiari. Baadhi ya wataalamu hawa na walioyasema kuhusu mada hii ya upanuzi wa kisitiari ni kama wafuatao. Hock na Joseph (1996) wanaeleza kuwa matumizi ya sitiari ni mbinu moja kuu ambayo kwayo maneno hupata maana mpya na pana zaidi katika lugha. Maelezo haya ya Hock na Joseph (hapo njuu) yana maana kuwa maneno hupanuka kimatumizi kwa kuongezewa maana zingine tofauti na maana za awali kwa kutumia mbinu ya kisitiari. Mbali na maelezo ya wataalamu wengine kuhusu upanuzi wa kisitiari maelezo haya yatatucaa katika tasnifu hii.

Anusu (2017) kuhusu kipengele hiki cha upanuzi wa kileksika ulio wa kisitiari anasema kuwa katika badiliko hili, wazo moja linaloashiriwa na neno au kirai linatumika pia kuashiria neno au kirai kingine kuonyesha mfanano uliopo baina ya hayo maneno au kirai.

Cuddon (1979) anasema kuwa katika upanuzi wa kisitiari maana ya tamko inayowasilishwa ni tofauti na maana wazi ya tamko hilo moja. Yamkinika kuwa maelezo haya ya Cuddon yana uzito na ndio maana Simuyu (2016) anatoa maelezo ya dhana hii yanayofanana rupia kwa ya pili na

haya maelezo ya Cuddon (hapo juu) anayesema pia kuwa katika mchakato huu wa upanuzi wa kisitiari maana ya neno ipo mbali na maana wazi kumaanisha maana ya neno fulani kimkutadha na kiisimu haifanani kwa kuwa katika upanuzi huu wa kisitiari maana halisi ya neno inahamishwa kutoka kwa kuashiria kitu kimoja hadi kuashiria dhana au kitu kingine.

Mfano;

(44) Azam FC ndiyo *jogoo* wa kandanda nchini Tanzania.

Neno jogoo ambaye ni njimbi linasimba dhana jogoo. Msomaji wa magazeti anapolipata neno hili limetumika katika muktadha wa mchezo wa kandanda yeze hulazimika kuunda dhana za dharura kama vile, jogoo ni mnyama, ni aina ya ndege, hufugwa na binadamu, ni kuku dume na huwika kila asubuhi alfajiri na mapema. Aitchson (2003) anasema kuwa vikoa vya kisemantiki vina utofauti na msikilizaji huashiriwa kufananisha vitu vinavyohusika kimatendo ili aweze kufasiri kifungu cha maneno ambacho kinahusika. Kwa sababu ya tofauti ya kisemantiki iliyopo kuwa kuku dume na wachezaji wa timu ya Azam FC kuwa binadanu inalazimisha msomaji wa magazeti kuhusu mchezo wa kandanda akaufanye mfanyiko huu wa upanuzi wa kisitiari ili aweze kuufasiri ujumbe ulioko kweneye maandishi kuhusu mchezo wa kandanda.

Msomaji au msikilizaji wa kandanda au anapolisoma au kulisikia neno hili katika muktadha wa kandanda maana wazi inayomkujia akilini mwake ni ile ya aina ya ndege na pia ni kuku dume huwika kila asubuhi. Kwa sababu timu ya Azam FC inayorejelewa na mwandishi wa gazeti haiwezi shindwa na timu yoyote nchini Tanzania, inakuwa ni rahisi kwa msomaji kuweza kufasiri maana inayokusudiwa na mwandishi. Maoni haya yanalandana na fikra za Aitchison (2003) anayefafanua hali hii kwa kusema kuwa katika sampuli ya kiasili, vitu ambavyo hufananishwa vina uwezo wa kuwa tofauti kwa kuwa vikoa vyao vya kisemantiki ni tofauti na kufanana kwao ni kule kwa kuashiria sifa chache za kawaida kufanana. Hivyo basi msomaji anachukua sifa moja ya jogoo na hadi kwa wachezaji wa timu ya Azam FC na kuunda dhana ya dharura ya jogoo. Hatimaye, msomaji anafasiri maandishi au matamko ya mtangazaji kuwa Azam FC ni hodari kuliko timu zingine nchini Tanzania kwa kuwa jogoo huchukuiwa na binadamu kuwa hodari kwa sababu ya kuwapanda kuku wa kike.

(45) Niyonzima *kifaru* cha Tanzania anafunga bao la kwanza msikilizaji.

*Kifaru* ni aina ya mnyama mwenye nguvu nyingi zaidi na ambaye kiulinganishi yumo katika kundi la wanyama watano bora. Kutokana na nguvu zake zilizokithiri, *kifaru* anaweza kufanya mambo makubwa na mazito ambayo wenyama wengine hawezu kufanya. Neno lili hili *kifaru* limepanuliwa maana na kutumika kwa kifaa cha kupigania vita ambacho hupita popote pasina na kusuiliwa. Kutokana na sifa hizi Niyonzima anapoitwa *kifaru* cha Warwanda, ina mana kwamba yeze ni mchezaji wa Warwanda aliye na nguvu na kwa hivyo nguvu zake zimemuwezesha kufunga bao. Katiika mfano huu kumetumika mzungu wa lugha ambao ni upanuzi wa kistiari.

### **3.2 4 Chuku**

Dhana ya chuku ni moja ya mizungu ya lugha inayotumika kutia ladha mazungumzo au maandishi. Kwa mujibu wa Wilson (2003) chuku ni badiliko la upanuzi wa kileksika ambalo linahusisha kiwango kikubwa cha upanuzi wa maana na hivyo kusababisha dhana iliyosimbwa kutengana kwa kiasi kikubwa na dhana inayowasilishwa. Tunakubaliana na maelezo haya na kuongeza kuwa kipengele hiki cha upanuzi wa maana kileksika kinahusisha kutia chumvi na kupiga chuku maneno au hali na hii huwa haimanishi maana kuchukuliwa hivyo waziwazi. Kwa mfano;

(46) Msikilizaji ni katika uwanja wa Kasarani jijini Nairobi ambapo timu ya Gor Mahia na AFC Leopards kwa jina lingine inafahamika kama Ingwe karibu kuingia uwanjani, leo ni ile siku msikilizaji tutajua *mbichi* na *mbivu* baina ya timu hizi za nchini Kenya.

Dhana iliyosimbwa na neno *mbichi* ni MBICHI na neno *mbivu* linasimba dhana MBIVU. Kwa mujibu wa TUKI (2013) neno *mbichi* lina maana ya kutofika upeo wa kukomaa na kuwa tayari kuliwa kama vile maembe, machungwa na ndizi vilevile *mbichi* ina maana ya chakula kilichopikwa kutofika kiwango cha kuliwa na watu. Kitende iva kina maana ya kuwa *mbivu*; penvuka kama vile matunda, pikika na kuwa tayari chakula kwa ajili ya kuliwa, na pia kuwa tayari kwa jambo lilikowa linaandaliwa. Msikilizaji wa mchezo wa kandanda anaposikia maneno haya yakitumika katika utangazaji wa mchezo wa kandanda hulazimika kuunda dhana za dharura kama vile matunda *mbichi* hayajafika kiwango cha kukomaa, hayaliwi, yana uchachu, chakula *mbichi* hakijafika kiwango cha kuliwa na hivyo hakiliwi, matunda ambayo yameiva yanaliwa, chakula ambacho kimepikwa na kimeiva kiko yayari kuliwa. Hata hivyo maana hii ni wazi mno kuliko ile mtangazaji anamaanisha katika muktadha huu wa utangazaji wa mchezo wa kandanda. Kwa kuwa timu ya mchezo wa kandanda haiwezi kuwa *mbichi* ama *mbivu* ili isiwe tayari kuliwa

wala kuwa mbivu ndio iwe tayari kuliwa ina maana kuwa hapa kuna kutia chumvi. Mtangazaji anaposema kuwa watajua timu mbichi ni gani anajaribu kuhamisha maana ya chakula ambacho kimepikwa na hakijafika kiwango cha kuliwa au matunda kama vile maembe ambayo hayajakomaa na kufika kiwango cha kuliwa kwa ile timu ambayo anarejelea kama ambayo haifai kushinda mchezo huu kwa kukosa ukomavu. Dhana ya mbichi hutumiwa pamoja na mbivu ili kuonyesha kwamba hizi ni dhana ambazo ni vinyume. Kwa hali hii basi, mtangazaji anaposema watajua timu mbivu ni gani anajaribu vilevile kuhamisha maana ya matunda yaliyopevuka na kuwa tayari kuliwa na chakula ambacho kimepikwa hadi kikawa tayari kuliwa kwa timu anayoirejelea kama inayostahili kushinda. Kwa kurejelea muktadha wa maneno haya ambao ni utangazaji wa mchezo wa kandanda tuna uwezo wa kufasiri maana ya maneno haya. Timu itakayoshindwa kwa kufungwa magoli mengi kwa kuwa haina ujuzi wa kufunga magoli kurejelewa na mtangazaji kuwa *mbichi* na ile timu itakayoshinda nyingine kwa kuifunga magoli mengi kwa kuwa ina ujuzi wa kufunga magoli kurejelewa kama *mbivu*.

(47) Simba FC imekuwa *katili* kwa wiki kadha sasa. Ilizoa ushindi wake wa tano mfululizo katikati mwa wiki.

Dhana iliyosimbwa na neno katili ni KATILI. Neno katili lina maana ya siokuwa na huruma; dhalimu, kaini, mwovu, nduli. Msomaji wa gazeti au msikilizaji wa habari kuhusu mchezo wa kandanda anapokutana na neno hili likitumika katika muktadha wa mchezo wa kandanda hulazimika kuunda dhana za dharura kwa haraka iwezekanavyo ili aweze kuufasiri maana inayokusudiwa kuwasilishwa na mwandishi au mtangazaji. Msomaji au msikilizaji ataunda dhana za dharura kama vile kuna timu ambayo ni dhalimu, timu yenye haina huruma, timu yenye inatendea nyingine maovu. Maana hii ni ya wazi mno na sio ile mwandishi au mtangazaji wa habari za kandanda alikusudia kuwasilisha kwa wasomaji au wasikilizaji wa magazeti kuhusu mchezo wa kandanda. Msomaji atalazimika kufanya mchakato wa chuku ili aweze kuufasiri maana. Kulingana na muktadha wa matumizi ya neno katili, kwa kufanya mchakato wa chuku msomaji au msikilizaji atafasiri maana ya neno katili kuwa timu hiyo ya Juventus kuibuka washindi kwa kuwalaza wapinzani wao bila huruma. Kitendo hiki cha kuibuka washindi kinatiwa chumvi au kupigwa chuku.

Bloomfield (1933) anaeleza kuwa katika mchakato huu wa chuku, maana za maneno zenye nguvu zinahamishwa katika maneno mengine na kuwa na maana ambazo hazina nguvu yaani

legevu. Maana asilia za maneno mbivu, mbichi na katili ambayo ndiyo mifano tumeitoa katika mchakato huu wa chuku, maana zao asilia zina nguvu ikilinganishwa na zile maana ambazo zinawasilishwa na maneno haya katika lugha ya kandanda. Hii ni kwa sababu maana asilia na maana zao katika lugha ya kandanda zinatofautiana kwa kiwango kikubwa.

### **3.2.5 Kisio la Maana**

Katika kipengele hiki cha upanuzi wa maana za maneno, Wilson (2003) anasema kuwa tamko lililo na maana thabitilinatanuliwa hadi kwa kivuli cha hali na ambapo hali hizi ziko nje ya maana halisi mahususi ya tamko katika lugha husika. Katika badiliko hili, kuna tofauti kubwa sana kati ya dhana iliyosimbwa kisemantiki na dhana ambayo inawasilishwa katika tamko. Wilson (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa misamiati ya kijiografia, misamiati iliyoelezwa kwa njia ya ukarusho na matumizi legevu ya takwimu za kukadiria ni mifano mizuri katika badiliko hili la upanuzi wa maana.

Kwa mfano;

(48) Msikilizaji ni mechiki kati ya Simba FC na Azam FC ambayo imehudhuriwa na *mamilioni ya watu*.

*Mamilioni ya watu* ni halaiki ya watu ambayo kihali halisi haiwezi kutoshea katika viwanja vya kandanda hasa katika mataifa ya Ulimwengu wa Tatu kukiwemo Kenya na Tanzania. Tujuavyo ni kwamba, viwanja vya mataifa haya huweza kutosheleza laki kadhaa tu za watu. Kwa kutaja *mamilioni ya watu* maana inayojitokeza ni kwamba ni watu wengi waliohudhuria na wala si wachache.

(49) Ni katika uwanja wa Kasarani jijini Nairobi ambapo mashabiki *wengi* wa timu ya Gor Mahia na wa Wazito FC wamefika ili kushabikia timu hizi katika mechiki ya leo msikilizaji.

Katika mfano huu, kisio la maana linalojitokeza ni kwamba mashabiki waliohudhuria mechiki si wachache.

Katika mifano hii tulioitoa kumetumika makadirio ya idadi na ambayo si wazi maana yanamwachia msikilizaji au mtazamaji kutoa maamuzi yake kuhusu idadi ya wale waliohudhuria mchezo huu wa kandanda. Kwa hali hii basi tunaweza kusema kuwa lugha ya kandanda katika Kiswahili hutumia vilevile mbinu hii ya kisio la maana ili kupanua maana za kileksimu.

### **3.2.6 Upanuzi wa Kategoria**

Neno la kategoria mahususi ambalo linatambulika sana na wanajamii linatanuliwa kimaana na kuanza kutumika na wanajamii wote ambapo kitu hicho kinatumiwa (Wilson 2003). Katika utafiti huu, tunakubaliana na maelezo haya na kuongeza kwamba, maana ya neno inayowasilishwa na neno hilo linapoanza kutumiwa na wanajamii wote huwa tofauti na ile maana ambayo imesimbwa kisemantiki na neno husika.

Katika badiliko hili la upanuzi wa maana nomino za kawaida na nomino za kipekee ndizo ambazo huchangia katika badiliko hili. Kwa mfano, majina ya Chomsky na Shakespear (Glucksberg, 2001) yanaashiria waandishi sifika na tajika katika ulimwengu wa sarufi na fasihi mtawalia. Kwa hali hii mtu akitajwa kama Shakespear itakuwa na maana kwamba yeche na mwandishi mzuri wa kazi za fasihi na za kiubunilizi kwa jumla. Mfano;

(50) Haruna Niyonzima *baba, baba mzazi* Niyonzima anapiga mpira upande wa Morrison.

(51) Bao linafungwa na Wafula wa AFC Leopards katika dakika ya ishirini na nane nakwambia msikilizaji huyu ni *Messi* wa Afrika.

Katika mfano wa kwanza, *baba* ni nomino ya kawaida. Nomino hii ina maana ya *mzazi* mwanamume. Katika mchezo huu wa kandanda, dhana ya baba imetumika kuonyesha ubabe na uhodari wa mchezaji huyu Niyonzima. Hapa kumefanyika badiliko la upanuzi wa kategoria.

Katika mfano wa pili neno *Messi* ni nomino ya kipekee. *Messi* ni mchezaji wa kandanda katika bara Ulaya ambaye anajulikana ulimwenguni kote kwa ujuzi wake wa kufunga mabao. Mchezaji huyu anaaminika kuwa ndiye mchezaji ambaye ameweza kufunga magoli mengi kuliko wote kwa sasa. Jina lake linatumika kurejelea Wafula ambaye ameifungia timu ya AFC Leopards mabao na kwa hivyo msikilizaji anaufasiri ujumbe huu kuwa, katika timu hii ya AFC Leopards mchezaji Wafula ndiye ameweza kuifungia timu hiyo mabao mengi ikilinganishwa na wachezaji wengine wote.

### **3.2.7 Ubunaji wa Maana Mpya na Uundaji wa Kileksimu**

Ubunaji wa maana mpya na uundaji wa kileksimu ni mchakato wa nadharia ya pragmatiki leksika ambao unahusisha leksimu ambazo tayari ziko katika lugha fulani mahususi zinaongezewa viambishi awali au tamati na kuunda leksimu mpya na ambazo zinasababisha ubunaji wa maana mpya katika lugha hiyo husika. Kwa mfano, neno *udume* kuundwa kutokana

na neno *ndume*, neno *mbabe*, *wababe* na *ubabe* kuundwa kutokana na neno *baba*, *mame* kutokana na neno *mama*.

Mfano;

(52) *Mababe wa KPL wapisha timu 48 kuanza matayarisho ya kandanda.*

Katika mfano huu, neno *baba* limeongezewa kiambishi awali [ma] na kiambishi tamati [e] ili kuunda neno *mababe* ambalo katika muktadha wa kandanda linasimamia mabingwa na wachezaji wasioweza kushindwa. Katika mfano huu, kumetumika mbinu ya upanuzi wa maana za kileksimu ambayo ni ubunaji wa maana mpya na uundaji wa kileksimu.

### **3.3 Hitimisho**

Katika sura hii, tumejadili namna maneno ya lugha ya Kiswahili yanavyopata mabadiliko ya kisemantiki huku tukirejelea lugha ya kandanda nchini Kenya na Tanzania. Mabadiliko haya ni upanuzi na ubanaji wa maana za maneno. Vilevile, tumeweza kuchanganua mabadiliko haya ya upanuzi na ubanaji kwa kutumia mihimili na michakato ya pragmatiki leksika. Mihihimi tulioitumia ni semantiki kileksika ambayo inashughulikia maana za maneno na dhana za dharura ambazo zinaundwa na msikilizaji wakati wa kuelewa tamko. Michakato ya pragmatiki iliyotumika ni ubanaji wa maana kileksika, upanuzi wa kileksika, chuku, upanuzi wa kategoria, kisio la maana, ubanaji wa maana mpya na uundaji wa kileksimu. Katika uchanganuzi wetu tuligundua kuwa, maneno yanayopata mabadiliko ya ubanaji wa maana ni machache ikilinganishwa na yale yanayopata mabadiliko ya upanuzi wa maana.

Imebainika kwamba, kuna matumizi mengi ya upanuzi wa maana kuliko yale ya ubanaji wa maana katika utangazaji wa kandanda katika nchi zote mbili za Kenya na Tanzania. Sababu ya kimsingi inayopelekea upanuzi wa maana kujitokeza kwa wingi ni kasi ya kandanda kama mchezo ambapo kasi hii haimpi wakati mtangazaji kutafuta neno asilia na kile anachotaka kukisema. Mabadiliko haya ya upanuzi na ubanaji wa maana yamejitokeza hasa katika kategoria za maneno zilizo za nomino na vitenzi. Yumkini, vitenzi vinatumika kwa sababu mchezo wa kandanda ni mchezo unaofanywa kimatendo.

## **SURA YA NNE**

### **SABABU NA MIKAKATI YA MABADILIKO YA KISEMANTIKI KATIKA LUGHA YA KANDANDA**

#### **4.1 Utangulizi**

Katika sura ya tatu, tumejadili namna maneno ya lugha ya Kiswahili yanavyopata mabadiliko ya kisemantiki huku tukirejelea lugha ya kandanda nchini Kenya na Tanzania. Mabadiliko haya ni upanuzi na ubanaji wa maana za maneno. Kutohana na uchanganuzi wetu, tulipata kuwa maneno yanayopata mabadiliko ya ubanaji wa maana ni machache ikilinganishwa na yale yanayopata mabadiliko ya upanuzi wa maana.

Kutokana na mbinu zetu za utafiti ambazo zilihusu usikilizaji pamoja na usomaji wa habari za matangazo ya kandanda, katika sura hii tunaangazia sababu za mabadiliko ya kisemantiki katika lugha ya kandanda kama inavyojidhihirisha kutokana na utangazaji wa mchezo huu nchini Kenya na Tanzania. Lengo kuu la sura hii ni kueleza sababu na mikakati inayopelekea mabadiliko ya kisemantiki kutokea katika utangazaji wa lugha ya kandanda nchini Kenya na Tanzania kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Kutokana na data yetu, sababu na mikakati ifuatayo ndiyo ilisababisha mabadiliko ya kisemantiki katika Kiswahili kwa kurejelea lugha ya kandanda.

#### **4.1.1 Upolisemia**

Kwa kurejelea lugha ya kandanda kama inavyotumika nchini Kenya na Tanzania, tuligundua kwamba kuna upolisemia katika matumizi ya maneno ambayo kihali halisi huwa ni ya maana moja au zaidi. Hali hii ilitegemea muktadha wa kile kilichokuwa kikijili au uelewa aliayoutaka uwafikie walengwa wa neno husika katika utangazaji wa kandanda. Kwa mfano;

(53) Bao limefungwa msikilizaji na mchezaji wa timu ya Gor Mahia. Kwa hakika Arocho

*Si mchawi.*

Katika kauli hii kuna wingi wa maana ambao ni upolisemia uliojitokeza kwa sababu mchawi huroga watu wakafa na kwa sababu hii watu walio na shida ya kusumbuliwa huwaendea ili wawaondolee shida hiyo. Hata hivyo, katika utangazaji wa kandanda ambapo Arocho ni mtangazaji yeye amebashiri kuwa bao litafungwa na hivyo ndivyo inavyokuwa. Kwa hali hii Arocho akisema chochote kinachukuliwa kama Kuruani ambacho ni kitabu takatifu kwa Waisilamu na kwa hiyo neno lake linachukuliwa kama ukweli mtupu.

#### **4.1.2 Mazingira**

Dhana ya mazingira katika muktadha wa utangazaji wa kandanda ni suala linalohusu sajili ya kandanda kama ilivyo kwa sajili yoyote ile. Sajili ya kandanda inatumia lugha kutegemea mazingira yake. Kwa hali hii, lugha ya kandanda inajibainisha iliyo spesheli kwa sababu ya mazingira inamojikuta. Kwa mfano;

(54) Ni dakika kumi na tano zimepita msikilizaji bao la kwanza linafungwa na Mayele wa timu ya Yanga. Nakwambia msikilizaji huyu ni *mbabe* wa soka.

Neno mbabe limetumika katika mchezo wa kandanda kuonyesha umahiri wa mhusika.

#### **4.1.3 Urahisishaji wa Mazungumzo**

Mtangazaji anapokuwa katika harakati za kutangaza kandanda inayokwenda kwa kasi hawi na wakati wa kuzingatia masuala ya kaida za lugha na kwa hiyo hujisemea mambo ili kurahisisha kazi yake ya utangazaji wa kandanda. Hali hii ndiyo tunayoita urahisishaji wa mazungumzo. Kwa mfano;

(55) Oluoch! Oluoch! Oluoch!

Mtangazaji wa kandanda alisikika akitaja jina la mchezaji pekee aliyeitwa Oluoch kwa sababu alikuwa anawapiga chenga wapinzani wake akikaribia kufunga bao. Huu ni usisitizaji wa mtangazaji ili kurahisisha mazungumzo baina yake na msikilizaji.

#### **4.1.4 Analojia.**

Analojia inahusu uchukuliaji wa maana kutokana na maana za hapo awali. Analojia kama dhana inaweza kugawika kuwili ambapo kuna analojia hasa au timilifu na analojia chukulizi au isiyo ya ukweli. Katika mchezo wa kandanda kama tulivyoshuhudia kutokana na utafiti wetu aina hizi mbili zilijitokeza. Kwanza, kulitumika maneno kama mchawi kwa maana ya mtu anayefanya mambo ya kiajabu ajabu na ambayo binadamu wa kawaida hawezu kuelewa au kuamini kurejelea mtabiri wa bao lilofungwa. Katika sentensi ya (53) Arocho si *mchawi*. Pili, kuhusu analojia isiyo ya ukweli, mfano ufuatao ulijitokeza;

(57) Mpira *umempiga chenga* mchezaji wa Yanga.

Kupiga chenga ni sifa ya kitu kilicho hai lakini katika muktadha wa mchezo wa kandanda mpira umepewa uhai na hii ni sifa isiyokuwa ya mpira kwa kuwa ni dude tu lililotiwa hewa. Ni kwa mantiki hii ambapo tunasema kwamba kumetumika mbinu ya tashhisi na analojia isiyokuwa ya ukweli.

#### **4.1.5 Utahozi**

Utahozi au utohoaji ni mbinu ya lugha inayohusu ukopaji wa msamiati kutoka lugha moja hadi nyingine. Utahozi huashiria mahusiano ya kihistoria na kitamaduni ambayo yamekuwepo baina ya lugha husika. Katika muktadha wa utangazaji wa kandanda watangazaji hukopa maneno mengi kutoka lugha ya Kiingereza ikilinganishwa na lugha zingine. Kwa mfano;

(58) Msikilizaji leo ni mechii baina ya *timu* ya Tusker na Gor Mahia na Gor Mahia tayari imefunga *goli* moja huku Tusker wakiwa na sufuri.

Maneno *timu* na *goli* yametoholewa kutoka lugha ya Kiingereza ambayo ni *team* na *goal* na kutumika katika utangazaji wa kandanda kwa Kiswahili.

#### **4.1.6 Utiaji wa Misamiati Mipyä**

Lugha kama ulio utamaduni ni kitu hai ambacho hubadilika kila uchao. Kwa sababu hii, lugha ya kandanda huonyesha mabadiliko haya ya kimsamiati kila uchao. Hii ina maana kuwa msamiati wa kandanda uliotumika miaka ishirini niliyopita si ule unaotumika sasa bali kuna utowekaji, uingizwaji na hata utumizi sambamba wa msamiati wa zamani na wa sasa. Kutokana na utafiti wetu, tulipata mfano ufuatao;

(59) Olunga msikilizaji nakwambia *amemlalia yombo* mchezaji wa Tusker.

Msemo *amemlalia yombo* umetoweka na badala yake kunatumika *amemchezea manuwari* kama inavyotumika nchini Kenya sasa. Hili ni badiliko la kisemantiki na linalotokana na mapisi ya wakati.

#### **4.1.7 Kunyambua Maneno**

Lugha ya Kiswahili ni lugha ambishi bainishi. Kutokana na hali hii, lugha hii huweza kuambisha viambishi mbalimbali kwa mizizi wa neno ili kujitokeza na maana ambazo mhusika huwa amekusudia kujitokeza nazo. Hali hii vilevile hujitokeza katika mchezo wa kandanda Kiswahili kinapotumika. Utafiti wetu, ulibaini maneno kama vile;

(60) *Ameulalia* mpira mchezaji wa Simba.

Neno *lala* katika muktadha huu na ambalo ni kitenzi limenyambuliwa na kuwa *lalia* ili kuleta maana aliyoikusudia mtangazaji.

#### **4.1.8 Kufupisha Maneno/Akronimu**

Lugha yoyote ile hutumia ufupishaji wa maneno ili kusemea kitu kwa urahisi bila kwenda mzunguko. Lugha ya Kiswahili na utangazaji wake wa kandanda haikuachwa nje kwa hili. Lugha hii inatoha maneno ya Kiingereza na kuyafupisha. Kwa mfano;

(61) Timu ya AFC Leopards hajawezza kufunga bao lolote msikilizaji nakwambia *kipa* wa Gor Mahia ako macho sana.

Neno *goalkeeper* la Kiingereza linatoholewa na kuwa *golikipa* lakini kwa sababu ya kutaka kurahisisha matamshi na kutofautisha maana linafupishwa na mtangazaji wa kandanda na

kutumia *kipa* pekee. Huu ni mfano wa ufupishaji wa neno lililotoholewa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili.

#### **4.1.9 Kuambatanisha Maneno**

Uambatanishaji kama dhana ya uundaji wa msamiati katika lugha uhusu uunganishaji pamoja wa maneno mawili au zaidi katika lugha ili kuunda neno moja la kusimamia dhana fulani. Maneno haya yanayounganishwa si lazima yaweze kuashiria moja kwa moja maana lengwa kwa dhana husika. Kwa mfano;

(62) Msikilizaji karibu katika uwanja wa Kasarani ambapo *wanakandanda* wa timu ya Tusker na Gor Mahia watajua mshindi ni nani.

Neno wanakandanda limeundwa kutokana na maneno mawili ambayo yako katika Kiswahili na yana maana tofauti. Maneno hayo yameambatanishwa na kuunda neno moja.

#### **4.1.10 Urudiaji wa Maneno**

Urudiaji wa maneno hujulikana vilevile kama uradidi. Hii ni mbinu ya kisemantiki ambayo hulenga kukariri na kusitiza maana inayokusudiwa. Katika mchezo wa kandanda hali hii hujitokeza pale ambapo mpira unakwenda kwa kasi na kwa hiyo mtangazaji hana nafasi ya kutosha ya kuzingatia sarufi na vilevile urudiaji hujitokeza pale ambapo mtangazaji anaepuka kupoteza muda kwa kusema kila tukio kwa sababu ya muda anao. Kwa mfano;

(63) Otieno...Otieno...Otieno anachenga.... anachenga mpira. Kweli ni mchezaji hatari.

Kutokana na mfano hapo juu mtangazaji wa kandanda alirudia maneno kwa kuwa alikuwa anaepuka kupoteza muda kwa kusema kila tukio kwa sababu ya muda anao.

### **4.3 Hitimisho**

Katika sura hii, tumeleza sababu za mabadiliko ya kisemantiki kwa kurejelea lugha ya utangazaji wa kandanda nchini Kenya na Tanzania. Sababu na mikakati ambayo tumeeleza ni upolisemia, mazingira, urahisishaji wa mazungumzo, analogia, utohozi, utiaji wa misamiati mipya ili itumike sambamba na misamiati ya zamani, kunyambua maneno, kufupisha maneno na urudiaji wa maneno. Katika uchanganuzi wetu tuligundua kuwa, sababu na mikakati ya mabadiliko ya kisemantiki ilitokea nchini Kenya na Tanzania kwa kurejelea lugha ya kandanda katika Kiswahili.

Katika kuchunguza sababu za mabadiliko ya kisemantiki katika mchezo wa kandanda, imebainika kuwa hakuna tofauti za kimsingi baina ya sababu za utokeaji wa mabadiliko haya katika mataifa ya Kenya na Tanzania. Sababu ya kiisimu inayoweza kutolewa ni kwamba kuna kufululiza kwa lugha ya Kiswahili baina ya mataifa haya yanayopakana.

## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI WA MATOKEO, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1. Utangulizi**

Utafiti huu umekuwa na lengo la kuweka wazi namna mabadiliko ya kisemantiki ambayo ni ubanaji na upanuzi hutokea katika Kiswahili. Imedhihirika kwamba upanuzi na ubanaji wa maana za maneno unatokea katika Kiswahili nchini Kenya na Tanzania. Mabadiliko haya tumeyaeleza kwa kurejelea mifano tulioikusanya kutoka kwa mtandao wa *YouTube* na magazeti ya Kenya na Tanzania. Katika utafiti huu, tumeongozwa na Nadharia ya Pragmatiki Leksika na data yetu imechananuliwa kwa kutumia nadharia hii na pia katika kuainisha aina za mabadiliko ya maana.

Kazi hii ya utafiti imegawika sura tano ambapo sura ya kwanza ni utangulizi wa jumla ya utafiti wetu na ambao umezingatia mambo yafuatayo: Usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti pamoja na nadharia iliyotumika katika kazi hii na hatimaye mbinu za utafiti.

Sura ya pili imekuwa ni kuhusu sajili ya kandanda katika ujumla wake. Katika sura hii tumelinganisha na kulinganua vipengele mbalimbali vya utangazajiji wa mpira wa kandanda nchini Kenya na Tanzania. Imejibainisha kuwa japo kuna tofauti za hapa na pale hasa kimazungumzo kuna usambamba mwingi kimaandishi.

Sura ya tatu inahusu mabadiliko ya kisemantiki yanayoikumba lugha ya Kiswahili inapotumika katika utangazaji wa mchezo wa kandanda nchini Kenya na Tanzania. Katika sura hii, tumejadili namna maneno ya lugha ya Kiswahili yanavyopata mabadiliko ya kisemantiki huku tukirejelea lugha ya kandanda nchini Kenya na Tanzania. Mabadiliko haya ni upanuzi na ubanaji wa maana za maneno. Vilevile, tumeweza kuchanganua mabadiliko haya ya upanuzi na ubanaji kwa kutumia mihimili na michakato ya pragmatiki leksika. Mihihili tulioitumia ni semantiki kileksika ambayo inashughulikia maana za maneno na dhana za dharura ambazo zinaundwa na msikilizaji wakati wa kuelewa tamko. Michakato ya pragmatiki iliyotumika ni ubanaji wa maana kileksika, upanuzi wa kileksika, chuku, upanuzi wa kategoria, kisio la maana, ubunaji wa maana mpya na uundaji wa kileksimu. Katika uchanganuzi wetu tuligundua kuwa, maneno yanayopata mabadiliko ya ubanaji wa maana ni machache ikilinganishwa na yale yanayopata mabadiliko ya upanuzi wa maana.

Imebainika kwamba, kuna matumizi mengi ya upanuzi wa maana kuliko yale ya ubanaji wa maana katika utangazaji wa kandanda katika nchi zote mbili za Kenya na Tanzania. Sababu ya kimsingi inayopelekea upanuzi wa maana kujitokeza kwa wingi ni kasi ya kandanda kama mchezo ambapo kasi hii haimpi mtangazaji kutafuta neno asilia na kile anachotaka kukisema. Mabadiliko haya ya upanuzi na ubanaji wa maana yamejitokeza hasa katika kategoria za maneno zilizo za nomino na vitenzi. Yumkini, vitenzi vinatumika kwa sababu mchezo wa kandanda ni mchezo unaofanywa kimatendo.

Sura ya nne inahusu sababu na mikakati ya mabadiliko ya kisemantiki. Katika sura hii, tumeeleza sababu za mabadiliko ya kisemantiki kwa kurejelea lugha ya utangazaji wa kandanda nchini Kenya na Tanzania. Sababu na mikakati ambayo tumeeleza ni upolisemia, mazingira, urahisishaji wa mazungumzo, athari za lugha ya mama, analogia, utohozi, utiaji wa misamiati mipyi ili itumike sambamba na misamiati ya zamani, kunyambua maneno, kufupisha maneno na urudiaji wa maneno.

Katika kuchunguza sababu za mabadiliko ya kisemantiki katika mchezo wa kandanda, imebainika kuwa hakuna tofauti za kimsingi baina ya sababu za utokeaji wa mabadiliko haya katika mataifa ya Kenya na Tanzania. Sababu ya kiisimu inayoweza kutolewa ni kwamba kuna kufululiza kwa lugha ya Kiswahili baina ya mataifa haya yanayopakana.

Kisha sura hii ya tano inahusu muhtasari wa matokeo, mahitimisho na mapendekezo kwa ajili ya tafiti za baadaye kuhusiana na mada yetu ya utafiti.

## **5.2. Muhtasari wa Matokeo**

Data tulioikusanya kwa ajili ya utafiti huu imeonyesha kuwa kuna tofauti baina ya lugha ya kandanda inayotumika nchini Kenya na Tanzania. Kuhusu uchanganyaji msimbo watangazaji wa kandanda nchini Kenya huegemea zaidi katika Kiingereza kuliko wale wa Tanzania ambao nao pia huegemea zaidi katika Kiarabu kwa sababu mchezo huu unapokwenda kwa kasi lugha inayotumika pia huwa ya kasi na kuwa na hali ya kuchanganya ndimi na kutia bwembwe kwa upande wa mtangazaji. Aidha, uhawilishaji msimbo hufanyika zaidi katika nchi ya Kenya kuliko ilivyo Tanzania. Watangazaji wa kandanda nchini Kenya hawazungumzi kwa lafudhi isiyo sanifu ikilinganishwa na watangazaji wa kandanda nchini Tanzania.

Katika utafiti huu, imetokea kwamba upanuzi na ubanaji hujitokeza kote Kenya na Tanzania na sababu za hali hii ziliweza kujibainisha wazi. Vilevile, athari za ubanaji na upanuzi wa maana za maneno zimeweza kujitokeza kama ambazo zinaathiri mawasiliano kama vile maana iliyokusudiwa inaweza isijitokeze kama ilivyodhamiriwa kwa upande wa hadhira lengwa.

Katika utafiti huu, imetokea kwamba sababu za kiisimu zilisababisha mabadiliko ya kisemantiki ambayo ni upanuzi na ubanaji wa maana za maneno. Tulishughulikia sababu na mikakati ambayo ni upolisemia, mazingira, urahisishaji wa mazungumzo, athari za lugha ya kwanza, analogia, utohozi, utiaji wa misamiati mipyä, kufupisha maneno na kuambatanisha maneno. Kwa kurejelea lugha ya kandanda kama inavyotumika nchini Kenya na Tanzania, tuligundua kwamba kuna upolisemia katika matumizi ya maneno ambayo kihali halisi huwa ni ya maana moja au zaidi. Hali hii ilitegemea muktadha wa kile kilichokuwa kikijili au uelewa alioutaka uwafikie walengwa wa neno husika katika utangazaji wa kandanda.

Dhana ya mazingira katika muktadha wa utangazaji wa kandanda ni suala linalohusu sajili ya kandanda kama ilivyo kwa sajili yoyote ile. Sajili ya kandanda inatumia lugha kutegemea

mazingira yake. Kwa hali hii, lugha ya kandanda inajibainisha iliyo spesheli kwa sababu ya mazingira inamojikuta.

Mtangazaji anapokuwa katika harakati za kutangaza kandanda inayokwenda kwa kasi hawi na wakati wa kuzingatia masuala ya kaida za lugha na kwa hiyo hujisemea mambo ili kurahisisha kazi yake ya utangazaji wa kandanda. Hali hii ndiyo tunayoita urahisishaji wa mazungumzo

Analojia inahusu uchukuliaji wa maana kutokana na maana za hapo awali. Analojia kama dhana inaweza kugawika kuwili ambapo kuna analogia hasa au timilifu na analogia chukulizi au isiyo ya ukweli. Katika mchezo wa kandanda kama tulivyoshuhudia kutokana na utafiti wetu aina hizi mbili zilijitokeza.

Utohozi au utohoaji ni mbinu ya lugha inayohusu ukopaji wa msamiati kutoka lugha moja hadi nyingine. Utohozi huashiria mahusiano ya kihistoria na kitamaduni ambayo yamekuwepo baina ya lugha husika. Katika muktadha wa utangazaji wa kandanda watangazaji hukopa maneno mengi kutoka lugha ya Kiingereza ikilinganishwa na lugha zingine.

Lugha kama ulio utamaduni ni kitu hai ambacho hubadilika kila uchao. Kwa sababu hii, lugha ya kandanda huonyesha mabadiliko haya ya kimsamiati kila uchao. Hii ina maana kuwa msamiati wa kandanda uliotumika miaka ishirini iliyopita si ule unaotumika sasa bali kuna utowekaji, uingizwaji na hata utumizi sambamba wa msamiati wa zamani na wa sasa.

Lugha ya Kiswahili ni lugha ambishi bainishi. Kutokana na hali hii, lugha hii huweza kuambisha viambishi mbalimbali kwa mizizi wa neno ili kujitokeza na maana ambazo mhusika huwa amekusudia kujitokeza nazo. Hali hii vilevile hujitokeza katika mchezo wa kandanda Kiswahili kinapotumika.

Urudiaji wa maneno hujulikana vilevile kama uradidi. Katika mchezo wa kandanda hali hii hujitokeza pale ambapo mpira unakwenda kwa kasi na kwa hiyo mtangazaji hana nafasi ya kutosha ya kuzingatia sarufi na vilevile hujitokeza pale ambapo mtangazaji anaepuka kupoteza muda kwa kusema kila tukio kwa sababu ya muda anao.

Lugha yoyote ile hutumia ufupishaji wa maneno ili kusemea kitu kwa urahisi bila kwenda mzunguko. Lugha ya Kiswahili na utangazaji wake wa kandanda haikuachwa nje kwa hili. Lugha hii inatoho maneno ya Kiingereza na kuyafupisha.

### **5.3. Mapendekezo**

Kiswahili ni lugha ya jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo inatumika kama lugha sambazi. Kihistoria, Kenya na Tanzania zina itikadi tofauti za kisiasa na kwa hiyo matumizi ya msamiati katika nchi hizi ni tofauti. Kwa hali hii, tunapendekeza kufanywe utafiti kuhusu utofauti na mfanano wa msamiati katika sajili mbalimbali baina ya mataifa haya mawili ili watumizi wa Kiswahili waweze kufahamu ili waweze kurahisisha mawasiliano. Hii ni kwa sababu, katika utafiti wetu tulichunguza mfanano na utofauti wa msamiati baina ya mataifa yaliyotajwa kwa kujikita katika sajili ya kandanda.

Katika utafiti wetu, tumechunguza mabadiliko ya kisemantiki ambayo ni ubanaji na upanuzi wa maana katika utangazaji wa mchezo wa kandanda kwa kujikita katika mataifa mawili ambayo ni Kenya na Tanzania. Tumejikita katika kueleza maana mpya za maneno zinazoibuka wakati wa utangazaji wa mchezo wa kandanda tofauti na maana inayozoleka au kujulikana, hivyo basi hatukuweza kushughulikia etimolojia ya maneno hayo. Tunapendekeza utafiti uweze kufanywa utakaochunguza etimolojia ya maneno yanayotumika katika utangazaji wa kandanda katika Kiswahili.

## **MAREJELEO**

Aitchison, J. (2003) *Words in the Mind: An Introduction to the Mental Lexicon*. Oxford.

Blackwell Publishing.

Anusu, J. (2017) Usawazishaji wa Leksimu katika Kiswahili: Utafiti Kifani wa Vihiga. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).

Berk- Seligson, S. (1886) Linguistic Constraints on Intra-Sentential Code-Switching: A Sudy of Spanish/Hebrew Bilingualism. *Language in Society*15:313-348.

Binyanya, R.M. (2014) Sajili ya Maafisa wa Polisi: Tathmini ya Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Katika Kituo cha Polisi cha Central, Nairobi. Chuo Kikuu Cha Nairobi. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).

Bloomfield, L. (1933) Language. In *Open Journal of Linguistics* (18: 167-180). New York: Holt, Reinhart and Winston (Eds).

Blutner, R. (2011) Some Perspectives on Lexical Pragmatics. In *Journal of Pragmatics Reader* (15:1-38) London: Routlegde.

Blutner, R. (1998) Lexical Pragmatics in *Journal of Semantics* 15:115-162.

Briely, S. (1955) *The Advertising Handbook*. London: Routledge.

- Budejovice, C. (2015) Legicxicoloal View of the Language of the Sport Commentaries. University of South Bohemia. M.A. Thesis. (Haijachapishwa).
- Buliba, A., Njogu, K. na Mwihaki, A. (2006) *Isimujamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Chapman, R. (1989) *Linguistics and Literature. An Introduction to Literary Studies*. London: Edward Arnold.
- Crystal, D. & Davy, D. (1969). *Investigating English style*. London: Longman Group Limited.
- Crystal, D. (1977) *A Dictionary of Linguistics and Phonetics*. Oxford (UK): Blackwell Publishers.
- Cuddon, J.A. (1979) *A Dictionary of Literary Terms*. Great Britain: Andre Deutch Limited.
- Deuchal, M na Quay, S. (2000) *Bilingual Acquisition: Theoretical Implications of A Case Study*. New York: Oxford University Press.
- Glucksberg, S. (2001). *Understanding Figurative Language: From Metaphors to Idioms*. Oxford: Oxford University Press.
- Hock, H.H. & Joseph, B.D. (1996) *Language History, Language Change and Language Relationships: An Introduction to Historical and Comparative Linguistics*. Mouton de Gruyter.
- Humpolik, R. (2014) Language of Football Commentators: An Analysis of Live English Football Commentary and its Types. Masaryk University. M.A Thesis. (Haijachapishwa)
- Hymes, H. (1974) *Foundations in Sociolinguistics: An Ethnographic Approach*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.
- Ipara, O. na Maina, G. (2008) *Fani ya Isimujamii kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Oxford University Press.
- Iribemwangi, P.I. & A. Mukhwana (2011) *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers.
- 
- (2010) *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele*. University of Nairobi.

- Lucass, F.L. (1955) *Style*. London: Cassell & Company
- Marisya, P. (2017) Mchango wa Sajili ya Kidini katika Kufanikisha Riwaya mbili za Ken Walibora (Kidaga Kimemwozea na Ndoto ya Almasi). Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).
- Muchura, W. (2004) Textual Function of Women Advertisement Magazines. University of Nairobi. M.A. Thesis. (Haijachapishwa).
- Mugenda, O. M. & Mugenda, A.G. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.
- Mukhwana, A. (1990) Siasa na Uimarikaji wa Kiswahili Kenya. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa)
- Muysken, P. (2000) *Bilingual Speech. A typology of code-switching*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Nandama, K.S. (2004) Kubadilisha Msimbo Katika Bunge la Kenya. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).
- Ngure, A. (2003) *Fasihi simulizi kwa shule za sekondari*. Nairobi. Phoenix Publishers Ltd.
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi. The Jomo Kenyatta Foundation.
- Njimu, B. (2015) Lexical Adjustments in Sports-Writing in the Three Kenyan Newspapers. University of Nairobi. M.A. Thesis. (Haijachapishwa).
- Poplack, S. (1980) "Sometimes I will start a Sentence in Spanish y termino en Espanol: Toward a Typology of Code-Switching." *Linguistics 18*. pp58-618
- Oiro, G. O (2017) Urudiaji na Uwasilishaji wa Maana Katika Ushairi wa Kisasa. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa)
- Okoth, O.P. (2018) Uchanganuzi wa Matumizi ya Agoti za Wafungwa: Hali ya Magereza Teule katika Jimbo la Kisumu, Kenya. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa)

- Okuku, W.M. (2010) Uchanganuzi wa Kiisimu wa Baadhi ya Matini za Kiswahili Mtazamo wa Pragmatiki Leksika. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa)
- Otieno, M.B. (2014) Use of Language in Sports Headlines Reporting Soccer in Kenya. Chuo Kikuu cha Nairobi. M.A. Thesis. (Haijachapishwa).
- Rajab, W.T. (2017) Tathmini ya Mabadiliko ya Maana ya Msamiati wa Kiswahili Katika Muktadha wa Kisiasa.: Mifano Kutoka Katika Hotuba za Kampeni Uchaguzi wa 2015. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).
- Shaviya, L. M. (2015) Uchanganuzi wa Kiisimu wa Baadhi ya Semi Katika Matini ya Kidini: Mtazamo wa Pragmatiki. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa).
- Simiyu, C.N. (2016) The Portrayal of men and women in selected Bukusu Circumsition Songs: A Lexical Pragmatic Approach. University of Nairobi. M.A. Thesis (Haijachapishwa).
- Simiyu, J.N. (2010) Nafasi Ya Ulinganifu Wa Kipragmatiki Katika Tafsiri Za Makala Za Mchezo Wa Kandanda Magazetini. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa)
- Sweetser, E. (1990) *From Etimology to Pragmatics: Metaphorical and Cultural Aspects of Semantic Structure*. Cambridge University Press. Cambridge.
- Trudgil, P. (1974) *The Social Differentiation of English in Norwich*. Cambridge: Cambridge University Press.
- TUKI, (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lughha*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors Ltd.
- Wamitila, K.W. (2001) *Kamusi ya Methali*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi yas Tashbihi, Vitendawili, Milio na Mishangao*: Longhorn Publishers.
- Wamitila, K.W. (2004) *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.
- Wamitila, K.W. (2008) *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Warambo, P. (2011) Uchanganuzi wa Maendeleo ya Kisemantiki katika Sheng: Mtazamo wa Pragmatiki Leksika. Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A.(Haijachapishwa).

Wilson, D. (2003) *Relevance and Lexical Pragmatics* in *Italian Journal of Linguistics* 15.2:273-291

Wilson, D.&R.Carston, (2007) *A unitary approach to lexical Pragmatics.: Relevance, inference and ad hoc concepts* from <http://www.phoc.ucl.ac.uk/home/deirdre/index3.html> 17.4.2017, 1:20 na sekunde tisa, usiku, saa za Afrika Mashariki.